Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu.
Kwa siku zilizohesabiwa. Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine. Na wale wanaoweza, watoe fidia kwa kumlisha maskini... (2:184 - 185)

JUZU 75 No. 185 | RAMDH./SHAWWAL 1437 | JUNI/JULAI 2016 | IHSAN/WAFA 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu aeleza falsafa ya saumu na kusema:

Fungeni kwa kutafuta Uchamungu tu

Na Mwandishi wetu

Dar es Salaam

Muhtasari wa Hotuba ya Hadhrat Khalifatul masih V a.t.b.a. katika Sala ya Ijumaa ya 3 Juni 2016

Khalifa Mtukufu alizungumzia juu ya Maswala mbalimbali yahusuyo Ramadhan

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Inshallah ndani ya siku chache zijazo mwezi wenye baraka wa Ramadhani utaanza.

Pamoja na kwamba katika baadhi ya nchi siku hizi mchana ni mrefu sana na hivyo kufunga saumu kunakuwa kugumu, hata hivyo kufunga saumu ni lazima kwa wale walio wakubwa na ambao wana afya.



HadhratMasroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a.

Katika nchi ambazo mchana ni mkubwa sana hadi masaa 22 au 23 wafungaji wa nchi hizo wapange muda wao wa kula daku na kufuturu kwa kutumia majira ya nchi za jirani, vinginevyo hakutokuwa na muda wa daku, wala futari, wala muda wa Tahajjud, Sala ya Alfajr au Sala ya Isha.

Kufunga ni moja ya nguzo za msingi za Islam. Kuna baadhi ya maswali yanayoulizwa kuhusu saumu, muda wa kula daku, muda wa kufuturu na hukumu ya kufunga mtu akiwa mgonjwa au safarini. Kwa fadhili za Allah maelfu ya watu wanajiunga na Jumuiya kila mwaka wengine wakitokea madhehebu mbalimbali za Kiislamu na wengine wakitokea nje ya Islam. Tunao wajibu wa kuwapatia hawa wote majibu muafaka ya maswali hayo ili mioyoni mwao musibaki wasiwasi na wapate utulivu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitumwa akiwa hakimu muadilifu. Alikuwa aje atoe maamuzi ya maswali yote yatakayojitokeza kuhusu misingi ya Islam. Alifafanua haya yote na kutupatia majibu na hivyo ni wajibu wetu kuangalia maamuzi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.katika kila tatizo. Leo nitafafanua kufusu maoni na maamuzi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.juu ya maswali mbalimbali kuhusu saumu na tuelewe

Endelea uk. 3

Serikali inajali huduma za Taasisi za Kidini - Waziri Mkuu

Na Jamil Mwanga
Dar es Salaam

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa ameelezea kufurahishwa kwake baada ya kukutana na ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania uliokwenda kumtembelea nyumbani kwake jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Waziri Mkuu alisema kuwa ziara ya ujumbe wa Ahmadiyya inathibitisha ukweli kuwa Serikali inashikamana na madhehebu ya dini na ipo tayari kuwasikiliza na kushirikiana nayo katika kutatua kero za wananchi.



Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akimkabidhi Qur'an Tukufu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa

"Wapo wanaoamini kuwa Serikali yetu haishikamani na madhehebu ya dini, nimefarijika kukutana nanyi na kwa niaba ya Serikali tutashirikiana kutatua matatizo ya wananchi", alisema.

Mapema Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya nchini aliyeongoza ujumbe huo alimweleza Waziri Mkuu kuwa Jumuiya ya Ahmadiyya mbali na kujihusisha na kazi za kiroho pia imekuwa

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

LAILATUL QADRI YA KWELI

Lailatul Qadir ni Istilahi maarufu masikioni mwa Waislamu, kwani Allah Mwenyewe Ameitaja ndani ya Quran Tukufu akizielekeza hisia zetu kwenye Baraka kubwa miongoni mwa Baraka zake zinazoambatana na ushukaji wa Quran tukufu.

Mtukufu Mtume s.a.w. naye ameisisitiza neema hii pale alipotuelekeza kuutafuta usiku wa Lailatul Qadr (Usiku Heshima) kwenye siku kumi za mwisho wa mwezi wa Ramadhani.

Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. nao walifanya bidii kubwa kuitafuta Lailatul Qadr na walikuwa na hamu ya kujichumia neema zake, kiasi hiki kwamba mke wa Mtume s.a.w. hadhrat Bibi Aisha r.a. alipata kumuuliza Mtume s.a.w., kama itokezee nigundue kwamba huu ni usiku wa Lailatul Qadr jee, niombe nini humo? Mtume s.a.w. akamjibu omba hivi: "Ee Mola wangu, U Msamehevu, Wapenda kusamehe, basi Nisamehe"

Hivyo Lailatul Qadr imekuwa ikiambatanishwa na neema na ufaulu mkubwa kwani inaaminika kwamba dua yoyote inayoombwa wakati huo huwa inakubaliwa moja kwa moja na Allah.
Kwa maana hii watu wamekuwa wakiinasibisha Lailatul Qadr na bahati kubwa kama vile utajiri na ufalme huku wengine wakiita 'Nyota ya Jaha'; na ndio si ajabu kusikia 'mtu fulani kaangukiwa na nyota ya jaha', na hata wasanii wa Unguja walipokuwa wakisubiria jambo fulani waliloliona kubwa mno kwao waliwahi kuimba "Silali naiongea, Lailatul Qadr"

Lakini Lailatul Qadri ni kitu gani?

Hili ndilo swali ambalo kila mwenye hamu ya Lailatul Qadr anapaswa kujiuliza, kwani bila kuelewa maana sahihi ya Lailatul Qadr huenda mtu akahaingaika kuitafuta maisha yake yote bila kuipata au kutosikia hata harufu yake!

Bila shaka ni muhimu kuielewa Lailatul Qadr ni kitu gani kabla ya kuingia kwenye juhudi za kuitafuta kwani zimekuwepo dhana mbali mbali za Lailatul Qadri hasa ni kitu gani. Wako wanaodhani kwamba Lailatul Qadri ni nyota ambayo inatoa mwanga mkali kiasi hiki kwamba ukibahatika kuiona basi dunia nzima kwako inakuwa inametameta kwa nuru na hapo unachoomba chochote hukubaliwa. Wale waamanio hivi huongeza kwamba unapoiona Lailatul Qadri usiombe mali kwa maana utapata mali nyingi kiasi cha kushindwa kuihesabu bali itakupoteza.
Wako wanaomani kwamba Lailatul Qadr sio nyota, bali ni usiku ambao kama umekubaliwa maombi yako basi unajisikia utulivu na amani ya nafsi kwa kiwango cha hali ya juu.

Imam wa zama, Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambaye ametumwa kuwa mfafanuzi wa mafundisho ya Islam katika zama hizi ametueleza maana ya kweli ya Lailatul Qadri.

Kwa ujumla, yeye ametueleza kwamba:
- Lailatul Qadri haina maana ya nyota yenye mwanga wala bahati ya kuangukiwa na donge la mali bali kwa hakika Lailatul Qadri ni muda ule katika maisha ambao mwaminio hupata mapinduzi ya kweli ndani ya moyo wake ya kumuondolea mapazia ya kiza na kumpatia nuru ya uwepo wa Allah.
- Lailatul Qadri ni muda ule ambao mtu hupata mabadiliko ya kuondokana na uzito wa kuyaelekea maamrisho ya Allah na kwake njia ya kumwendea Mola wake huwa rahisi mithili ya ndege apaaye angani.
- Lailatul Qadri ni muda ule ambao mtu hutanabahi juu ya lengo la kuumbwa kwake na akaamua kujitupa mbele ya kizingiti cha Mola wake kwa uaminifu wake wote.
- Lailatul Qadri ni ule wakati ambapo mja hupata yakini ya kuwepo kwa Allah na kuachana na miungu yote bandia ikiwemo nafsi yake mwenyewe na huviona vitu vingine vyote kana kwamba havipo na humtegemea Allah tu na katu hakitegemei kitu kingine chochote iwe utajiri, mamlaka au kipaji chochote.

Hizo ni katika maana za Lailatul Qadri zilizoelezwa na Imam wa zama.
Hiyo ndiyo Lailatul Qadri ambayo kila Muislamu anatakiwa ajitahidi kuipata. Na ni pale tu mtu atakapopata (***Lailatul Qadri hii***) mapinduzi ya kweli - ya kumubudu Mola wake ndipo katika kipindi hiki maisha yake yanapokuwa na thamani kuliko maisha ya mtu aliyeishi umri kamili wa mwanadamu ambao unakadiriwa kuwa miezi 1000 au wastani wa miaka themanini na kitu!
Allah Atujaalie kuipata Lailatul Qadri hii ndani ya maisha yetu.
Amin.

Serikali inajali huduma za Taasisi za Kidini



Ujumbe wa Ahmadiyya ukiongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, wakizungumza na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa nyumbani kwake, Dar es Salaam

Kutoka uk. 1

ikijitahidi kusaidia kutatua kero za kijamii hususan katika sekta za elimu, maji na afya. Sheikh Chaudhry alisema kupitia mradi wa "Humanity First" Jumuiya imetoa msaada wa mashine mbili za vifaa tiba (mammogram machines) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Aidha, imegawa kompyuta na vitabu katika baadhi ya shule katika Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam na mkoani Morogoro. Kuhusu huduma za maji, Jumuiya Ahmadiyya imesaidia kuchimba visima na kuweka pampu za maji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo vijiji vilivyoko mkoani Shinyanga.

Sheikh Chaudhry alimweleza Waziri Mkuu kuwa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya imekuwa mstari mbele kusisitiza suala la amani kitaifa na kimataifa. Akifafanua hilo, alisema kuwa Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifa Mtukufu wa Tano, (a.t.b.a) hivi karibuni ametembelea nchi za Scandinavia na amehutubia kuhusu suala la amani ya dunia. Amesema inasikitisha kuwa baadhi ya waislamu huuana wenyewe kwa wenyewe kutokana na msimamo mkali na kisingizio cha kufanya jihadi jambo ambalo sio mafundisho ya Islamu na kwamba Jumuiya Ahmadiyya inajiahidi kupambana na upotoshaji huu kwa kueleza mafundisho sahihi ya Islamu kwa mujibu wa Qurani Tukufu na mwenendo wa Mtume Mtukufu Muhammad S.A.W.
Aidha, alisema katika kusisitiza agenda ya amani, Jumuiya Ahmadiyya Tanzania imekuwa ikifanya mikutano ya amani nchini na kuwaalika watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa madhehebu ya dini, viongozi wa Serikali na wanasiasa. Mikutano kama hiyo imekwishafanyika katika mikoa ya Morogoro, Mwanza, Dar es Salaam na Shinyanga. Alisema kuwa mkutano mwingine wa amani unaandaliwa na umepangwa kufanyika mkoani Dodoma tarehe 13 Julai, 2016 ambapo pia alitumia fursa hiyo kumwalika Waziri Mkuu kuhudhuria mkutano huo.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu alisema kuwa amani ni suala nyeti na linahitaji kutiliwa mkazo na kwamba ni vyema Jumuiya Ahmadiyya ikaendelea na mipango yake ya kusisitiza amani ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi na kwa wanasiasa pia. "Amani ni suala la msingi hata kwa vyama vya siasa na ninapenda kuwahakikishia kuwa endeleeni na mipango yenu ya kusisitiza amani na kuhudumia jamii na Serikali iko nanyi bega kwa bega", alisisitiza.

Mwishoni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alikabidhiwa na Amir na Mbashiri Mkuu zawadi ya vitabu vya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ikiwemo Tafsiri ya Qur'ani Tukufu kwa lugha ya Kiswahili.

Endelea uk. 5

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Fungeni kwa kutafuta Uchamungu tu

Kutoka uk. 1

kwamba maamuzi yake ndiyo ya mwisho katika zama hizi. Tukumbuke kwamba kanuni nambari moja ya Islam ni taqwa. Hivyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Fungeni kwa uaminifu wote na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu.

Baadhi ya nyakati watoto huuliza kwa nini sisi tunaanza Ramadhani na kufungua tofauti na Waislamu wengine? Hakuna amri hiyo. Hatufanyi hivyo kwa makusudi na wala sio lazima siku zote iwe tofauti. Kuna nyakati ambapo tulikuwa tunafunga na kufungua siku moja. Katika nchi za kiislam au ambazo waislamu ni wengi kwa kawaida kuna kamati za kutangaza kuonekana kwa mwezi baada ya kujiridhisha. Katika nchi kama hizo sisi Waahmadiyya tunafunga na kuadhimisha Idi sawa na matangazo ya kamati hizo. Lakini katika nchi za magharibi hakuna kamati kama hizo wala tangazo rasmi kutoka serikalini, hivyo tunategemea kuonekana kwa mwandamo. Iwapo mahesabu yetu hayakwenda sawa, na mwandamo umeonekana kabla, tunaweza kuanza Ramadhani kabla, iwapo ushahidi umetolewa na mtu mchamungu. Kusema tu tuanze kufunga ili tuende sawa na wasio Waahmadiyya bila kuuona mwezi sio sahihi.

Huzur akasema Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameandika katika kitabu chake Surma Chasham Arya kuhusu hili: Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakupinga kufanya mahesabu kwa sababu hilo pia ni tawi la sayansi, lakini pia ameonesha umuhimu wa kuuona mwezi kwa uhalisia. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema "Mwenyezi Mungu amejaribu kurahisisha njia za kutekeleza amri kwa kuieleza jamii njia rahisi na za uwazi badala ya kuyafanya mambo kuwa magumu na yenye utata." Huzur alisema pia kutegemea tu mahesabu ya kamati za kutangaza mwezi kwamba mwandamo utakuwa siku ya 29 au 30 pia sio sahihi. Tunatakiwa tutegemee kuuona mwezi halisi. Pia Huzur alisema, Masihi Aliyeahidiwa a.s.amesema daima tusifuate tu mahesabu au nadharia. Makosa yanaweza kutokea. Ni jambo la wazi kwamba mtu asitegemee moja kwa moja juu ya sayansi bali pia afuate kuonekana kwa mwezi mwandamo. Pia mtu azingatie kwamba siku za kufunga hazizidi 30. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema "Kuuona mwezi ni jambo bora zaidi kuliko mahesabu. Baada ya kufanya uchunguzi wa kutosha juu ya hili, wanaulamaa wengi wa Ulaya wameonelea ni vyema kuushuhudia mwezi mwandamo."

Baadhi ya nyakati kuna uwezekano wa kutokea kosa. Masihi Aliyeahidiwa a.s.aliwahi kukabiliwa na hali hiyo. Rafiki mmoja kutoka Sialkot alimweleza Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba Ramadhani imeanza kwa kuchelewa hapa Qadian kuliko Sialkot ambako mwezi ulikuwa umeonekana kabla. Je tufanye nini maana siku moja itakuwa imepungua. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akajibu itabidi tufunge siku moja baada ya kumalizika kwa Ramadhani.

Kisha kuna swali la kula daku. Ni lazima kula daku kabla ya kufunga. Mtukufu Mtume s.a.w. aliamrisha kufanya hivyo. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema mtu ajitahidi kula daku kwani kuna baraka katika kufanya hivyo. Masihi Aliyeahidiwa a.s. na masahaba zake waliagizwa kula daku na kulikuwa na matayarisho maalum kwa wageni. Hazrat Sahibzada Mirza Bashir Ahmad Sahib r.a. ameandika kwamba Munshi Zafar Ahmad sahib wa Kapoorthala, alimwandikia kumweleza kwamba wakati alipokuwa akitembelea Qadian alikuwa akikaa chumba kilicho jirani na Masjid Mubarak. Siku moja alikuwa akila daku na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akapita karibu yake na kumuuliza unakula daku ya chapati na dengu? Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliwaita waandalizi na kuwauliza je hili ndilo daku ambalo tunawapatia marafiki zetu? Basi akawaagiza waandalizi kwamba wawaulize wale wote wanaofunga, juu ya daku wanalopendelea na matayarisho yafanywe. Msimamizi aliondoka na kuja na chakula nilichokipenda. Nilikuwa nimeshakula na adhana ikaanza kusomwa. Masihi Aliyeahidiwa a.s.akaniambia: Usiwe na wasiwasi endelea kula, kwani leo adhana imetolewa mapema.

Kuhusu kusali tahajjud na kula daku pamoja na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Hazrat Mirza Bashir Ahmad Sahib r.a. anasimulia kwamba Dr Mir Muhammad Ismail Sahib r.a alisema mnamo mwaka 1895, nilitumia mwezi wote wa Ramadhani nikiwa Qadian na nikasali Taraweeh au Tahajjud nyuma ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikwua akisali witri nyakati za mwanzoni mwa usiku na baadae kuamka na kusali rakaa 8 za tahajjud katika nyakati za mwisho wa usiku. Alikuwa akisoma Ayatul-Kursi katika Rakaa ya kwanza na Surah Ikhlaas katika rakaa ya pili. Pia alikuwa akisoma Ya Hayyo Ya Qayyum bi rahmatika astaghees kwenye Rukuu na Sujood. Alikuwa akisoma kwa namna ambayo nilikuwa nikimsiakia waziwazi. Kisha alikuwa akila daku baada ya tahajjud na alikuwa akiendelea kula hadi adhana inapomalizika. Hazrat Mirza Bashir Ahmad Sahib r.a. anasema hakuna mahusiano ya moja kwa moja kati ya adhana na kula daku. Hadi pale weupe wa asubuhi utakapoonekana mtu anaruhusiwa kuendelea na daku. Muda wa adhana unahusiana na muda wa sala. Sheria haiagizi kuacha kula kwa kusikia adhana. Wakati mtu wa kawaida anapoona kwamba kumepambazuka hapo ndipo aache kula daku. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema adhana inayotolewa na Bilal isikuzuieni kula daku hadi pale mtakaposikia adhana ya Ibn-e-Maktoum r.a. Ibn-e-Maktoum alikuwa kipofu na alikuwa akitoa adhana tu baada ya kuwasikia watu wakisema kwamba kumekucha.

Mwaka jana nilimweleza rafiki mmoja kwamba alikuwa anakula kwa kuchelewa sana na akaamua kufunga tena. Hakuhitajika kufunga tena iwapo anafuata mawazo ya hapo juu. Katika nchi za magharibi, kwa vile adhana haitolewi kwa sauti, kuna umuhimu wa kuona kwamba kumekucha.

Hazrat Mirza Bashiruddin sahib r.a. alisema kwamba katika mwaka 1903, Dr Khalifa Rashid ud Din sahib na mkewe r.a. walikuja Qadian na kubaki kwa siku nne. Wakaonyesha hamu yao ya kufunga wakiwa Qadian. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akawaletea daku ya chapati za Kashmiri, na akawahudumia yeye mwenyewe. Kisha akasikia adhana na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akawaambia Mwenyezi Mungu anasema katika Quran tukufu: "Na kuleni na kunweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe kutoka katika uzi mweusi wa alfajiri." (2:188)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. akasema watu hawafuati amri hii na hivyo kuwataka waendee kula wakati adhana inaendelea na pia akasema mwadhini siku hiyo aliadhini mapema.

Mtu anaweza kutumia chakula kizuri lakini kwa kiasi na mizania. Allah anasema katika Quran tukufu: "Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito ." (2:186)

Saumu imelazimishwa ili kuyarahisisha maisha ya mwaminio na kumwepusha na shida. Lakini baadhi ya watu wanaofikiria kwamba wanashinda na njaa mwezi wa Ramadhani, kwa hakika wanazitusi amri za Quran tukufu. Chakula hasa ni chakula cha kiroho, ambacho kinazirutubisha roho badala ya chakula cha kimwili kinachourutubisha mwili tu. Mtu anatakiwa ajitambue kwamba anafunga na hivyo ale kwa kiasi. Baadhi ya watu huishia kuongezeka uzito badala ya kupungua wakati wa ramadhani. Kwa baadhi ya watu mawazo yote yanakuwa ni kujaza matumbo yao tu badala ya saumu. Wanajilia tu vyakula vya mafuta mengi na tamtam kupita kiasi. Jambo hili hupunguza baraka za ramadhan. Kuna amri ya kuwahi kufuutru na kula daku na hayo ndio yenye baraka. Mtu anatakiwa kula chakula kizuri lakini kwa kiasi. Kufunga katika hali ya ugonjwa na safari kumekatazwa. Mirza Yaqub Baig Sahib anasema alikuja Qadian kutokea safarini wakati wa Alasiri na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamwambia afungue saumu. Pia alipoulizwa kuhusu ugonjwa alijibu, tunaamini kwamba ni lazima kujipatia faida ya ruhusa hiyo. Wale wasemao kwamba msafiri akiweza kufunga, afunge, Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema siioni kauli hiyo kuwa sahihi. Mohayyud din Ibn Arabi hakuona kuwa sawa kwa mtu kufunga akiwa safarini au mgonjwa, na alisema mtu anatakiwa kuzifunga tena siku hizo baadae. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akiwaruhusu wageni kufunga iwapo wanabakia Qadian. Alikuwa hawaruhusu kufunga siku wanayosafiri. Wakati jalsa ilipoangukia ramadhani, wageni walikuwa akipatiwa daku. Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakuwaruhusu watu kufunga wakiwa safarini lakini aliwaruhusu kufunga wale waliokuwa wakitembelea Qadian mara kwa mara na kukaa huko. Iwapo mtu anapanga kukaa sehemu fulani kwa zaidi ya siku 3 anatakiwa kufunga, lakini iwapo atakaa chini ya siku 3 anasamehewa.

Wakati Sheikh Muhammad Chaito alipotembelea Qadian, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alimuuliza iwapo alikuwa amefunga. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamwambia kwa vile alikuwa safarini na pia alikuwa mzee basi afungue saumu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akasema kutii tahafifu zilizotolewa na Quran pia ni sehemu ya uchamungu.

Kuhusiana na Msafiri au mgonjwa kufunga saumu, Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema ni kosa kufunga wakati mtu yu mgonjwa au yumo safarini. Kiini cha utawa ni kutii amri za Mwenyezi Mungu sio mtu kujipangia taratibu yeye mwenyewe. Hakuna utata, maagizo yapo wazi: "Hakuna kufunga wakati mtu yumo safarini au yu mgonjwa". Wakati mgeni huyu Baba Chaito ambaye hakuwa Ahmadiyya alipouliza je iwapo hakuna shida yoyote katika safari kwa nini mtu asifunge? Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamjibu hayo ni maoni yako mwenyewe.

Quran tukufu inasema "Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine" (2:185)

Quran tukufu haijafafanua ni safari ipi au ugonjwa upi. Pia mtu ashike njia inayoongoza kwenye taqwa.

Hazrat Maulvi Noor ud din r.a. alisema kwamba Ibn Arabi alisema kufunga baadae ni lazima hata kama mtu alifunga wakati akiwa safarini au mgonjwa. Kwani Mwenyezi Mungu amesema fungani siku za baadae muwapo wagonjwa au safarini. Hakuna maagizo kwamba utakapofunga ukiwa mgonjwa basi usifunge baadae. Yule anayefunga wakati yu mgonjwa basi anaasi amri ya Mwenyezi Mungu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema kwamba kama vile Mwenyezi Mungu alivyoamrisha kufunga saumu, pia ameamrisha kutokufunga katika mazingira fulani. Mtu anayefunga wakati yumo safarini au mgonjwa anatakiwa kufunga tena wakati atakapopata afya au safari yake kumalizika. Ni lazima kufuata amri hii ya Mwenyezi Mungu. Uokovu hupatikana kwa rehema ya Mungu na sio kwa kulazimisha. Mwenyezi Mungu hajafafanua kwamba mtu awe na ugonjaw mkubwa au mdogo au safari iwe fupi au ndefu.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akiwaeleza watu wafungue saumu zao iwapo walikuwa safarini. Alikuwa akisema, wakati Mwenyezi Mungu ameagiza msifunge muwapo safarini basi haifai kufunga. Wakati fulani ukiwa umebakia muda mfupi tu kabla ya muda wa futari, ilikuwa baada ya sala ya Alasiri Masihi Aliyeahidiwa a.s. alimwambia mgeni wake mmoja aliyekuwa msafiri afungue saumu. Mgeni akasema mbona muda uliobaki ni mfupi tu, lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s.akasema huwezi kumfurahisha Mwenyezi Mungu kwa kumlazimisha akubali saumu zako, bali kwa hakika Mwenyezi Mungu anakuwa radhi kwa sababu ya utii wako.

Katika ramadhani mojawapo, Masihi Aliyeahidiwa a.s.alitembelea Amristar. wakati akitoa hotuba bwana mmoja akampelekea chai, lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. akakataa. Yule bwana

Endelea uk. 4

Khilafat Rashida ya Mtume s.a.w.

Na Swahili Desk
Morogoro

Kutoka toleo lililopita

Baada ya vita hivyo vya ngamia Hadhrat Ali r.a. akamuasa Hadhrat Muawiya, aliyekuwa Gavana wa Syria, afanye Baiat ya utii kwake ili kuitakia mema Islam. Amir Muawiya akakataa kwa kisingizio cha kutaka kwanza kisasi cha Hadhrat Uthman r.a. aliyetokana pia na ukoo wa Umayya, kilipwe. Muawiya akisaidiwa na Amr bin Al "Asw wakaanza kutayarisha jeshi la uasi dhidi ya Hadhrat Ali r.a. Hapo akawa hana budi ila aelekee Syria kwenda kupambana na majeshi hayo ya uasi. Mnamo mwezi wa July mwaka wa 657 A.D. majeshi yao yakapambana katika vita vya Saffain. Maafa makubwa yalipatikana toka pande zote mbili. Muawiya alipoona anazidiwa akatunga hila ya kusitisha vita ili iundwe kamati ya waamuzi wa kutatua mzozo huo. Hadhrat Abu Musa Al Ash'ari akateuliwa kumuwakilisha Hadhrat Ali r.a. na Hadhrat Amr bin Al 'Asw kumuwakilisha Hadhrat Muawiya r.a.

Kwa bahati mbaya utatuzi huo ukashindikana kwa sababu Amr bin Al 'Aswalifanya hila ya kuepuka makubaliano aliyokubaliana na Abu Musa al Ash'ari. Kundi kubwa la watu ambao tangu mwanzo walipilipinga wazo hili la kuunda kamati ya waamuzi wakajitenga na Hadhrat Ali r.a. na kuunda kundi lao na kumchagua kiongozi wao. Kundi hili likajulikana kama Khawaarij yaani watu wa nje. Hadhrat Ali alijitahidi kuwashawishi waepukane na uasi huo bila mafanikio, na hatimaye vita kubwa ikapiganwa na Hadhrat Ali akawateketeza makhawaarij elfu themanini.

Baada ya kipigo hiki makhawaarij wakapanga njama za kuwaua Hadhrat Ali r.a., Muawiya na Amr bin al Asw kwa siku na wakati mmoja. Hadhrat Ali r.a alishambuliwa na kujeruhiwa vibaya wakati akielekea msikitini kwenye sala ya Al Fajiri na akafariki siku mbili baadaye. Amr na Muawiya walisalimika.

MIAKA MIA MOJA YA UKHALIFA WA KIAHMADIYYA NI USHAHIDI WA UKWELI WA MASIHI ALIYEAHIDIWA, HADHRAT MIRZA GHULAM AHMAD A.S., WA QADIAN

Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimari-shia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri.

Wale wanaofanywa kuwa Makhalifa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe huwa wanakuwa na sifa fulani zisizopatikana kwa watu wengine. Huteremkiwa na Malaika wanaowapasha habari za ghaibu toka kwa Mwenyezi Mungu, hupokelewa maombi yao zaidi kuliko wengine, hupatiwa msaada makhsus na Mwenyezi Mungu na majukumu yao hufanikiwa juu ya upinzani mkubwa usio na kifani waupatao.

Aya hii nimeyoisoma sasa hivi imebainisha wazi kabisa kuwa imani ya kweli na vitendo vinavyokubalika mbinguni vitathibitishwa kwa kustawi kwa nidhamu ya Ukhalifa ndani ya kundi husika, nidhamu kama ile iliyopatikana kwa manabii na mawalii waliopita kabla ya Islam. Sura Baqara : 31 na Swad : 27 zatuthibitishia kwamba unabii pia ni aina ya ukhalifa wa kuteuliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu, pale Mungu Aliposema kuwa Yeye Mwenyewe ndiye Atakayemuweka nabii Adam kuwa Khalifa katika ardhi, na hali kadhalika Akamuambia nabii Daud kuwa ni Yeye Mungu Mwenyewe, ndiye aliyemfanya Daud a.s. kuwa Khalifa katika ardhi na Kumuasa ahukumu baina ya watu kwa uadilifu.

Mtume Muhammad s.a.w. pia alitoa bishara ya ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa na kumsema kuwa atakuwa ni Hakimu Muadilifu, kama vile Mungu Alivyomfanya Daud kuwa Hakimu Muadilifu. Kuhusiana na Masihi Aliyeahidiwa Mtume s.a.w. aliwahi kusema: 'Alaa innahuu Khaliifatii fii ummatii', yaani, 'sikilizeni! yeye kwa hakika atakuwa ni Khalifa wangu ndani ya umati wangu', juu ya kwamba ndani ya Sahih Muslim, mara nne alimtaja Masihi Aliyeahidiwa kuwa atakuwa ni nabii wa Mwenyezi Mungu na atakuwa na masahaba na atafunuliwa Wahyi, lakini hata hivyo bado atakuwa ni Khalifa wake atakayetokana na umati wake. Kwa hiyo
nabii huwa anakuwa ni Khalifa wa kuteuliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu.

Sura Al Maida : 45 yatufafanulia kuwa Makhalifa, ambao baadhi yao walikuwa ni Manabii na baadhi yao hawakuwa manabii, bali wanazuoni tu na watawa, waliwahukumu wana wa Israeli kwa kutumia Taurati ambayo ilikuwa ni nuru na mwongozo kwa wana wa Israeli. Sasa kama Mungu Ametuahidi kuwa Atatufanya Makhalifa kama Alivyowafanya Makhalifa wale wa Kabla yetu, basi ni lazima kuwepo miongoni mwa wafuasi wa Mtume s.a.w. watakaokuwa Makhalifa wenye daraja la unabii, na wengine wao hawatakuwa na daraja la unabii, bali la uanazuoni na utawa, ambao msingi wa elimu yao utakuwa ni ufunuo wa Mwenyezi Mungu uliosababishwa na utakatifu wao na kuwa kwao na mawasiliano hai na Mwenyezi Mungu.

Dini ya Islam ilisemwa kuwa itaimarika kupitia nidhamu hiyo ya Ukhalifa, na ibada ya kweli isiyo na shirk ndani yake itapatikana ndani ya nidhamu hiyo hiyo ya ukhalifa, na Mwenyezi Mungu Ataibadili hofu ya wale waliomo ndani ya nidhamu hiyo kuwa amani. Na wale wote watakaoikataa na kuiasi nidhamu hiyo watakuwa ni wavunjao amri mbele ya Mwenyezi Mungu na mtume wake s.a.w.. Ndio sababu Mtume s.a.w. akasisitiza sana kwamba Waislamu watakaposikia habari za kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa basi ni lazima waende kuwa wafuasi wake hata kama itawabidi watambae juu ya theluji.

Mtume s.a.w. alitoa bishara kwamba mnamo siku za mwisho Isa mwana wa Mariamu atakuja duniani kuwahuisha Waislamu, kuihami na kuihubiri Islam, na kuwafanya watu wa dini zote waungane ndani ya dini moja ya Islam. Ujio huu wa Isa mara ya pili unafanana na ujio wa mara ya pili wa nabii Eliya ambapo ndani ya kitabu cha Malaki 4:5 ilibashiriwa kuwa Mtume Eliya atatumwa na Mwenyezi Mungu kabla ya kudhihiri kwa Masihi Yesu. Yesu alipodhihiri na kujitangaza kuwa ndiye Masihi, wanafunzi wake wakamuuliza mbona vitabu vinasema kuwa Eliya atakuja kwanza kabla ya Masihi? Ndipo alipowafunulia fumbo hilo kwa kuwaambia kuwa Yohana Mbatizaji ndiye aliyetimiza bishara ya ujio wa mara ya pili wa Eliya (Mathayo 11:14 na pia Mathayo 17:10-13 na Luka 1:17). Hapo Yesu akawa amefafanua kwa uwazi kabisa kuwa ujio wa mara ya pili wa nabii aliyekwisha fariki humaanisha ujio wa nabii mwingine anayefanana naye kiroho.

Mwenyezi Mungu Anapomteua Khalifa basi ni lazima Authibitishie ulimwengu kuwa Yeye Anawasiliana na mtu huyo kwa maongezi,

Endelea uk. 5

Fungeni kwa kutafuta Uchamungu tu

Kutoka uk. 3

aliposisitiza sana Masihi Aliyeahidiwa a.s. akachukua kikombe na kunywa kidogo. Wapinzani wakaanza kumtusi kwamba haiheshimu saumu. Baadhi wakamrushi mawe. Sheikh mmoja asiye Ahmadiyya akaleta kebehi kwa kusema: '"Leo watu wamemfanya Mirza kuwa mtume."

Kwa vile Mufti Fazl ur Rehman sahib ndiye aliyempatia chai Masihi Aliyeahidiwa a.s., watu wote walimchukia na wakaanza kumlaumu kwa tukio hilo. Wakati Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipoelezwa juu ya tukio hilo akasema hakufanya kosa lolote kwa kumpatia chai.

Wakati mmoja Masihi Aliyeahidiwa a.s. akiwa Ludhiana alikuwa amefunga na akaugua ghafla hadi kukuaribia kuzimia, hapo hapo akafungua saumu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akipendelea njia iliyo rahisi kati ya ruhusa mbili. Hadhrat bibi Aisha anasimulia hayo hayo kumhusu Mtukufu Mtume s.a.w. Baadhi ya nyakati Ramadhani inakuja wakati wa mavuno. Ni kipindi cha kazi ngumu kwa wakulima. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema matendo hulipwa kutokana na nia. Kila mtu anaweza kujitathimini mwenyewe juu ya msingi wa taqwa. Iwapo mtu atakosa mfanyakazi wa kumvunia, anaweza kukatisha saumu na kufunga baadae. Kwa wakati huo yeye atahesabiwa kuwa mongoni mwa wale wasioweza kufunga.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema, wakati fulani alianza kufikiria kwa nini kutoa Fidya ni lazima. Akasema ni kwa ajili ya kupata nguvu. Mtu anatoa Fidya ili apate nguvu kwani hili laweza kutokea kwa msaada wa Mwenyezi Mungu tu. Iwapo Mungu anapenda anaweza kumpatia nguvu hata mtu dhaifu. Mtu aombe kwa uchungu kwamba O Mola, huu ni mwezi wako ulioubariki, nami najisikia kupungukiwa kwa kushindwa kufunga na pia sina uhakika iwapo nitafika saumu ya mwaka ujao, au kwamba nitakuwa hai... Iwapo mtu ataomba kwa uaminifu, Mwenyezi Mungu ataupa nguvu moyo wake.

Fidya sio mbadala wa kufunga. Fidya ipo ya aina mbili. Ya muda mfupi na ya kudumu. Ya muda mfupi ni kwa wale wanaoweza kuja kufunga na ya kudumu ni kwa wale ambao hawana tena uwezo wa kufunga. Kima cha fidya ni chakula cha mtu mmoja. Kama Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakuweza kufunga alikuwa akitoa fidia na kufunga baadae. Kama mtu hawezi kufunga anaweza kumlisha maskini yeye mwenyewe au anaweza kuchangia kwenye mfuko wa mayatima huko Qadian.

Kama mtu atakula kwa kusahau hakuna adhabu bali anatakiwa aendelee kufunga. Watoto hawaruhusiwi kufunga kwa mujibu wa sharia. Wanaruhusiwa kufunga wanapokaribia umri wa kubaleghe. Mtu hatakiwi kuwafungisha watoto kwani ni kosa. Katika umri wa miaka 12 hadi 13 mtu awazoeshe watoto kufunga siku chache na ifikapo umri wa miaka 18 ndio mtu afunge kwa kudumu. Ni wajibu wa wazazi kuwazuia watoto wasifunge. Baadae watoto wakikua ndipo wazazi wawahimize kufunga. Umri wa miaka 18 umewekwa tu lakini katika maumbile ya baadhi ya watoto wanaweza wasiweze kufunga hadi miaka 21 sawa na hali yao ya kiafya. Binti mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa hapendi watoto wafunge kwa kudumu na baadhi ya nyakati alikuwa akimlazimisha kufungua kwa vile alikuwa mdogo.

Kuhusiana na Taraweeh: Ni ipi hukumu ya kusali rakaa 20. Sawa na sunna ya Mtukufu Mtume s.a.w. ni bora kusali rakaa 8 kwenye sehemu ya mwisho wa usiku, lakini pia inaweza kusaliwa mwanzoni mwake. Rakaa 20 na zaidi zilianzishwa baada ya mtukufu Mtume s.a.w.. Sunna ya Mtukufu Mtume s.a.w. ilikuwa ni kusali rakaa 8. Kama mtu yumo safarini anaweza kusali tarawehe peke yake. Kwa hakika Taraweeh ndio sala ya Tahajjud.

Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuielewa amri hii ya saumu na atubariki kutokana na ibada ya saumu na mwezi wa Ramadan, **Ameen.**

Khilafat Rashida ya Mtume s.a.w.

Kutoka uk. 4

na maneno ya Mungu huwa yanatoa pia bishara za mambo yatakayokuja dhihirika baadaye.

Mnamo karne ya kumi na tisa iliyoafikiana na karne ya kumi na nne ya Hijra, alidhihiri mja fulani wa Mwenyezi Mungu aliyekuwa na umri wa makamo, mwenye urefu wa kama futi 5 na nchi 8 hivi, rangi yake ikiwa ya ngano, macho yake yakiwa ni meusi na daima yalikuwa yakiinamia chini na yalionekana kama yasiyofumbuka kikamilifu kutokana na silika ya soni aliyokuwa nayo, mwenye sauti ya upole, mtawa sana na aliyejinasibisha kikamilifu na dini ya Islam, akiwa ni mja wa kweli wa Mwenyezi Mungu na mfuasi aliyejitokomeza ndani ya utii na upendo kwa Mtume Muhammad s.a.w.. Yeye aliutangazia ulimwengu kwamba kwa miaka kadhaa amekuwa akipokea ufunuo toka kwa Mwenyezi Mungu na kwamba Mungu Amemuambia kuwa siku ya kuhuika kwa Uislamu imekaribia na kwamba yeye ndiye amechaguliwa kulitekeleza jukumu hilo la kuistawisha na kuishindisha na kuieneza dini ya Islam duniani.

Sauti hii iliibukia katika mji mdogo sana wenye mamia tu ya wakazi, mji uliokuwepo ndani ya jimbo lililokuwa masikini kuliko yote katika majimbo ya India, likiwa halina kabisa miundo mbinu ya mawasiliano na sehemu zingine za Dunia. Mtu huyu alikuwa si mwingine bali Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian, aliyetokana na ukoo maarufu wa machifu, ambao kwa wakati huo ulikuwa umepoteza sehemu kubwa ya miliki yake. Alikuwa amepata elimu ya kawaida tu lakini aliisoma Kurani Tukufu kwa undani sana na hivyo kubarikiwa falsafa ya ndani kabisa ya elimu za kiroho.

Ufunuo aliofunuliwa, pamoja na mambo mengine, ulikuwa na ahadi kwamba Ujumbe huo, ambao Mwenyezi Mungu Amemkabidhi, utafikishwa hadi katika pembe zote za Dunia, na kwamba atabarikiwa kiasi hiki kwamba hata wafalme watatafuta baraka toka kwenye nguo zake, na kwamba mbegu ya uhuisho wa kiroho wa Islam aliyoipanda, itastawi na kuwa mti mkubwa ambao mizizi na matawi yake yataenea duniani kote, ambapo makundi ya watu yatabariz chini ya kivuli chake, na kwamba hakuna yeyote atakayeweza kuzuia mwendeleo huu ambao hatimaye sehemu kubwa ya wanadamu watakuwa wamepata hifadhi chini ya kivuli chake.

Mnamo mwaka 1864 Hadhrat Ahmad a.s. aliona njozi ya ajabu sana. Alimuona Mtume s.a.w. akiwa ameketi katika kiti cha enzi na yeye akiwa amesimama mbele yake kwa unyenyekevu akiwa ameshika kitabu kikubwa cha masuala ya kidini. Mtume Muhammad s.a.w. akamuuliza jina la kitabu kile alichokuwa Hadhrat Ahmad a.s. amekishika. Hadhrat Ahmad a.s. akamjibu kwa heshima kabisa kuwa kinaitwa 'Kutbii', kikiwa na maana kwamba ni kitabu ambacho hoja zake na dalili madhubuti, ziko imara na zisizotetereka kama nyota ya mbinguni. Hapo Mtume Muhammad s.a.w. akakishika kitabu hicho kama atakaye kukisoma. Mara kikageuka kuwa tunda tamu sana. Tunda hilo lilipokatwa vipande vidogo vidogo ili vigawanywe, asali ikatiririka kwa nguvu sana toka kwenye tunda hilo kiasi ya kwamba mikono yote ya Mtume s.a.w. ikalowana kabisa kwa asali hiyo. Wakati huo huo, kutokana na muujiza huo, maiti iliyokuwa nje ya mlango wa chumbani ikafufuka na kusimama nyuma ya Hadhrat Ahmad a.s. Yule mtu aliyefufuka alipokwisha kula sehemu yake ya tunda, Hadhrat Ahmad a.s. akaona kwamba jukwaa lile lililokuwa na kiti cha Mtume s.a.w. limeinuliwa juu toka kwenye sehemu yake ile ya mwanzo, wakati nuru iliyokuwa ikitoka kwenye uso wa Mtume s.a.w. ilikuwa ikienea pande zote.

Ndoto hii ilitimia baadae mnamo mwaka 1882 wakati Hadhrat Masihul Mau'ud a.s. alipoandika kitabu chake maarufu cha Barahiine Ahmadiyya, kitabu kilichosifika sana kama kitabu kilichothibitisha, kwa hoja zisizopingika, ubora, uzuri na ukweli wa Kurani Tukufu. Hadhrat Ahmad a.s. alitoa zawadi ya rupia elfu kumi kwa yeyote yule atakayeweza kuzivunja hoja zake alizozitoa ndani ya kitabu hicho. Islam ilihuika kwa hoja zilizokuwemo ndani ya kitabu hicho.

Mnamo tarehe 20 August 1886, alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu, kwa Fadhili na Huruma Yake, Amemfahamisha kuwa Atamjaalia mtoto wa kiume atakayekuwa na vipawa bora kabisa, vipawa ambavyo aliviorodhesha ndani ya tangazo lake hilo. Pia alisema kuwa mtoto huyo atafanana naye sana kwa uzuri na baraka. Huu ulikuwa ni ufunuo wenye sehemu nyingi. Na kweli mtoto huyo akazaliwa mnamo tarehe 12 January 1889.

Mnamo mwaka huo wa 1889 Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. akatangaza kwamba yeye ndiye Msuluhishi wa zama hizi aliyetumwa na Mungu kuja kuurekebisha ulimwengu, ambaye bishara ya kuja kwake ilitolewa na Mtume Muhammad s.a.w.. Mnamo mwezi March wa mwaka huo aliianzisha Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Wakati huo Wahyi (ufunuo) ulikuwa ukimteremkia kwa mfululizo. Akafahamishwa, kutokana na funuo hizo, kwamba yeye ndiye yule Imam Mahdi na Masihi Isa mwana wa Mariamu Aliyeahidiwa kufika katika zama hizi za mwisho kwa njia ya mfano, kama ule wa Yohana Mbatizaji kuja kwa mfano wa Eliya. Pia alifahamishwa ndani ya funuo hizo kwamba ujio wake umetimiza bishara zote za ujaji wa manabii mbali mbali wa dini mbali mbali ambao waliahidiwa kudhihiri mnamo siku hizi za mwisho, maarufu kama Aakhiruz zamaan.

Aliutangaza ufunuo alioupata toka kwa Mwenyezi Mungu uliosema: 'Mwenyezi Mungu Anataka kuanzisha Jumuiya ya watu waaminifu ambao watadhihirisha nguvu na taadhima ya Mwenyezi Mungu. Ataifanya Jumuiya hiyo ikue na kufanikiwa ili istawishe mapenzi ya Mwenyezi Mungu, ucha Mungu, utakaso, wema, amani na maelewano kati ya watu. Hao watakuwa ni kundi la watu waliojitupa kwa Mwenyezi Mungu. Atawaimarisha kwa roho Yake Mwenyewe na kuwabariki na kuwatakasa.' Pia alitangaza kuwa Mwenyezi Mungu Amempasha habari ya kwamba Jumuiya yake ya Waislamu wa Ahmadiyya itastawi mno na kuongezeka mara dufu. Maelfu ya watu watajiunga nayo, na Mungu Mwenyewe Ndiye Atakayewaangalia, na Ataifanya Jumuiya ikue kiasi ya kwamba wafuasi wake na maendeleo yake yataishangaza Dunia.

Madai yake haya yalizusha upinzani mkubwa sana na uadui dhidi yake, toka kwa viongozi wa kidini wa dini zote maarufu za wakati huo. Kadiri upinzani ulivyozidi dhidi yake ndivyo hivyo hivyo funuo za kimbingu zikawa zinazidi kumteremkia zikimhakikishia kuungwa kwake mkono na Allah, na mafanikio na ushindi. Aliweza kuwapata hapa na pale watu waliokuwa wacha Mungu na wenye kuyatafakari maandishi matakatifu na hoja za kimbingu, ambao hatimaye wakaungana naye na kuwa wafuasi wake. Idadi yao ikawa inaongezeka hadi kufikia idadi ya malaki katika uhai wake.

Alipewa hazina kubwa ya kiroho na kikhulka iliyodumu kumhakikishia ushindi na mafanikio juu ya kuwepo kila aina ya upinzani. Na ndivyo nidhamu za kimbingu huwa zinavyokuwa kwamba ushindi na mafanikio yake husababishwa na nguvu za kiroho na maadili mema, sio fedha wala utawala, ingawa hata vitu hivyo pia aliahidiwa na Mwenyezi Mungu kuwa vitapatikana kwa wingi, wakati msingi imara wa kiroho na kikhulka utakapokuwa umejengwa ndani ya mioyo ya wengi wa wafuasi wake, na hivyo kuepuka hatari ya kutekwa na kutawaliwa na tamaa za kidunia. Aliwaasa wafuasi wake watoe kipaumbele katika masuala ya kiroho kuliko yale ya kidunia.

Madai yake ya kupokea Wahyi toka kwa Mwenyezi Mungu yalimfanya aonekane, katika ulimwengu huu usio na habari na Mwenyezi Mungu, kuwa kichekesho kwa watu wa kidunia na kuwa shabaha ya dhihaka, kejeli na matusi.

Kudai kwake kwamba yeye ndiye yule kiongozi wa kiroho aliyeahidiwa na manabii waliopita wa dini mbali mbali, kufika katika zama za mwisha wa dunia, ziliibua chuki kubwa dhidi yake toka katika dini zote. Masheikh wa Kiislamu wakamtolea fatwa ya kumkufurisha na kutangaza kwamba yeyote atakayefanikiwa kumuua basi huyo atakuwa ameshajihakikishia pepo iliyojaa mahuurin 'ayn na mito ya asali na maziwa iliyofunikwa kwa vivuli vya miti ya mitende na mizaituni. Hatari zote hizi hazikumsumbua, kwani alishapata ahadi ya ulinzi toka kwa Mwenyezi Mungu pale alipomfunulia kuwa 'Atamlinda na madhara yote toka kwa watu'. Maisha yake yote yanatoa ushahidi wa ulinzi makhsus wa Mwenyezi Mungu. Hakuajiri mlinzi yeyote wa kumlinda.

Aliishi maisha matakatifu yasiyokuwa na doa lolote, akifuata nyayo za Mtume Muhammad s.a.w. Aliwapa changamoto wale wote waliomshutumu kwa uwongo wathibitishe kasoro yake yoyote ile ya kimaadili kabla ya madai yake na wakashindwa kufanya hivyo kama walivyoshindwa makafiri kufanya hivyo kwa Mtume Muhammad s.a.w.

Wahyi aliofunuliwa ulikuwa umejaa bishara nyingi zilizohusisha sehemu mbali mbali za dunia na kila aina ya maisha, ambazo zilitimia barabbara na kwa wakati wake hasa.
Alianzisha Jumuiya ambayo wafuasi wake walitakiwa wadhihirishe katika maisha yao sifa zote zile za kiroho na kimaadili zinazoagizwa na Islam na mfano mkubwa wa kuigwa ukiwa ni wa Mtume Muhammad s.a.w. Wafuasi wake wanatoka katika kila jamii ya watu. Wanatekeleza kila jukumu na kazi inayoruhusiwa katika dini, hawaishi kama wale waliojitenga kabisa na dunia na kuishi maisha ya kiajabu ajabu, bali wameonyesha mfano mzuri wa kuonewa gere, wa maisha yenye fanaka na baraka katika kila nyanja. Miongoni mwao alikuwemo mshindi wa zawadi ya nobel katika metaphysics, Professor Abdus Salaam, pia alikuwemo Raisi wa baraza kuu la Umoja wa Mataifa na Jaji wa Mahakama kuu ya Dunia, The Hague, Sir Muhammad Zafrullah Khan, pia alikuwemo Waziri wa Sheria wa Tanzania, Sheikh Amri Abedi Kaluta, mawaziri katika nchi mbali mbali, Majenerali wa Jeshi wa sifa zisizo za kawaida, Madaktari, Wanasayansi, mabilionea na mamilioni ya watu wa kawaida lakini wenye ucha Mungu usio wa kawaida, walioenea duniani kote kuanzia Amerika, Afrika, Ulaya, australia na Asia. Sifa zote hizi walizipata kutokana na mafundisho waliyoyapokea toka kwa Hadhrat Mirza Ghulam a.s. ambayo kwa hakika yalikuwa ndiyo mafundisho ya asili ya Mtume Muhammad s.a.w. aliyotuletea toka kwa Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih 2 r.a. anasimulia Ruya yake fulani kwa kusema : "Nilijiona katika Ruya niko msikitini ndani ya chumba cha Baitud Du'aa nikiwa nimeketi katika mkao wa Tashah hud (Attahiyyatu) huku
Nikiwa naomba dua hii; 'Yaa Ilahi naomba mwisho wangu uwe kama ulivyokuwa wa nabii Ibrahim a.s.' Halafu nikapandwa na jadhba na kusimama nikiwa naomba dua hii hii. Mara mlango ukafunguka nikamuona Mir Muhammad Ismail akiwa amesimama kizingutini huku akitoa miali ya nuru. Maana ya Ismail ni Mwenyezi Mungu Amesikia na mwisho wa kiibrahimu mradi wake ni kupata mwisho kama wa nabii Ibrahim a.s. kwamba alipofariki Mwenyezi Mungu aliwainua kuwa Makhalifa wake Hadhrat Ishaq na Hadhrat Ismail a.s. Hapa kuna bishara inayofanana ambapo mnapaswa mfurahie."

Mnamo tarehe 26 September 1909, Hadhrat Muslihul Mau'ud Khalifatul Masih wa pili r.a alisema kwamba:
'Mimi pia Mwenyezi Mungu Amenipasha habari Akisema: Nitakupatia mwana ambaye atakuwa Naasir (msaidizi) wa dini na atakayejifunga kibwebwe kuitumikia dini.' (Al Fazal 8 April 1915).

Ndani ya Talmud (Vitabu vya Hadithi za Wana wa Israel) kuna kauli isemayo kwamba baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa kufika katika zama za mwisho, ufalme wake wa kiroho utaenda kwa mwanawe halafu kwa mjukuu wake.
Ndani ya kitabu cha Haqiqatul Wahyi, Hadhrat Masihul Mau'ud a.s. anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia watoto wa kiume wanne na mjukuu wa kiume atakayezaliwa katika siku zijazo. Bishara hii ya mjukuu ilitimia wakati mwana wa Hadhrat Masihul Mau'ud a.s., Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad a.s., alipojaaliwa kupata mtoto wa kiume mnamo tarehe 16 November 1909. mtoto huyo alipewa jina la Nasir Ahmad, ambaye baadaye alikuja kuwa Khalifatul Masih wa tatu r.a. na kutimiza bishara hiyo ya Talmud.
Mwisho.

Bustani ya Washairi

ZINDUKENI ISILAMU ZINDUKENI

1 Enyi ndugu Isilamu, zindukeni
Muliopo hizi zamu, amkeni
Imeshafika taimu, sikieni
Zindukeni Isilamu, Zindukeni.

2 Imeshafika taimu, sikieni
Lile kundi maalumu, la kidini
Pweke la kiisilamu, tambuweni
Muhammad muadhamu, eleweni

3 Alolisema maalumu, abadani
Halingii Jahannamu, asilani
Na sababu mufahamu, hasa nini?
Hilo kundi si haramu, kwenye dini

4 Hilo kundi si haramu, kwenye dini
Limeundwa na karimu, madhumuni
Lifanye kazi muhimu, duniani
Kurejeshea kaumu, upya dini

5 Ilohama tufahamu, ya manani
Enyi ndugu Isilamu, zindukeni
Lishafika kundi lenu, la kidini
Jema la Kiisilamu, ingieni

6 Ingieni Isilamu, ingieni
Ingieni kundi lenu, ingieni
Kwenye makundi haramu, ya motoni
Ondokeni Isilamu, Jitoweni

7 Kwenye makundi haramu, Jitoweni
Yanomuasi karimu, yakwepeni
Dini yanayohujumu, ya manani
Yaliyojaa elimu, za vichwani

8 Yaliyojaa elimu, za vichwani
Zipotoshazo kaumu, za kubuni
Ondokeni Isilamu, ondokeni
Lishafika kundi lenu, Ingieni

9 Lishafika kundi lenu, la kidini
Jema la Kiisilamu, zindukeni
Lilotabiriwa kwenu, sikieni
Lishafika kwa kaumu, njooni

10 Njooni Isilamu, njooni
Ngieni kundini mwenu, ingieni
Hiyo ndo safina yenu, ingieni
Imeundwa na Karimu, zindukeni

11 Imeundwa na Karimu, Fahamuni
Na Nahodha maalumu, Hasa nani?
Ni mwana wa Mariamu, Tambuweni
Nabii wake Karimu, Eleweni

12 Ni nabii wa Karimu, Sikieni
Aliyepewa Isimu, Fahamuni
Ya mwana wa Mariamu, Zindukeni
Kabilaye maalumu, Muajemi

13 Kabilaye maalumu, muajemi
Karithi kubwa elimu, yenye shani
Ya kitabu cha Karimu, Qur'ani
Kajaa utaalamu, Kila fani

14 Kajaa utaalamu, kila fani
Vyema anaufahamu, usukani
Ana leseni maalumu, ya mbinguni
Amepewa na Karimu, si utani

15 Yenye muhuri maalumu, wake nani?
Wa Muhammad Mwadhamu, Eleweni
Lishafika kundi lenu, Liwahini
Liwahini Isilamu, Ingieni

16 Kwenye makundi haramu, Jitoweni
Wacheni kujidhulumu, Mtiini
Mtiini Mola wenu, Rahmani
Kaliunda kundi lenu, Ingieni

17 Mtiini Mola wenu, Rahmani
Kundi musilihasimu, Ingieni
Lipokeeni kwa hamu, Na imani
Na alama maalumu, Sikieni

18 Na alama maalumu, Zindukeni
Katuwekea Karimu, Fahamuni
Ya uongozi muhimu, Ulo chini
Ya mmoja uimamu, Wenye shani.

19 Ya mmoja uimamu, Wenye shani
Wa kurejesha kaumu, Kwenye dini
Upya ya Kiisilamu,Ilohuni
Lishafika kundi lenu, Njooni.

20 Njooni Isilamu, njooni
Njooni kundini mwenu, la kidini
Hiyo ndo safina yenu, tambueni
Ingieni Isilamu, mujihami

21 Hiyo ndo safina yenu, ingieni
Ingieni Isilamu, mujihami
Urudi umoja wenu, wa imani
Pamoja na nguvu zenu, za kidini

22 Urudi umoja wenu, wa imani
Pamoja na nguvu zenu, duniani
Ili ya Karimu, eleweni
Izishinde mufahamu, zote dini

23 Lishafika kundi lenu, ingieni
Na jinale maalumu, zindukeni
Laitwa Ahmadiyya, laitwa Ahmadiyya
Laitwa Ahmadiyya, ndilo jinale rasmi.

(Bimkubwa Kombo - Pemba)

KWANINI MWASEMA NO?

Bismillahi naanza, kwa hili ninalonena
Nataka kuwauliza, kwanini mnaukana
Ukhalifa wa aziza, uloletwa kutupona
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Kwa fadhila za aziza, sisi Ye katujaliza
Karne kuimaliza, na minane kuongeza
Watano kutuongoza, Khalifa wake muweza
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Mulibuni kwa dakika, mara tu kadisapia
Wetu sisi wa miaka, dunia yashuhudia
Twawapata kwa baraka, kutoka kwake Jalia
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Kiongoza waumini, kitabu chake manani
Chawabana kibaoni, kuwauliza kwanini?
Mwaipinga Qur'ani, dhidi ya hili jamani
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Aya zimefululiza, kutoka kwake Latwifa
Ila moja tosheleza, kutambua Ukhalifa
Lakini bado mwazoza, kuupinga Ukhalifa
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Suratul Annura, tano sita yaeleza
Watofanya yalo bora, kweli Atawajaliza
Kwani nyie sio bora, swali hili nauliza
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Khalifa kaahidiwa, toka miongoni mwetu
Kuja kutufunza njia, kumpata mola wetu
Kwa kufata manabia, enzi ya kizazi chetu
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Anopinga Qur'ani, basi huitwa kafiri
Mtanieleza nini, kunijibu swali hili
Ikiwa ni Qur'ani, inathibitisha hili
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

Ninawaaga kwaheri, wale wanao ukana
Nitungieni shairi, kunieleza bayana
Kwanini mwaukatiri, ukweli unonekana
Kwanini mwasema no? Ikiwa nyie hamna

(Zaidi Abdallah Machombe – DSM)

NI NANI WALIOUA?

Mhariri haujambo?, hali ninakujulia
Naomba muda kitambo, niwaeleze jamaa
Mwanza kumetuka jambo, lililoleta fadhaa
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Wameufanyia jambo, msikiti wa sunia
Wakatinga na mitambo, watu kuwashambulia
Manondo na mitarimbo, waumini kuwaua
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Tuwatumie mgambo, mabwana walioua
Wakomeshwe lao tambo, ukatili usofaa
Wafikishwe kwenye vyombo, wachukuliwe sheria
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Wasakwe kwenye malambo, kama wamejichimbia
Tusiwapambe mapambo, hao ni maharamia
Katu tusiende kombo, waovu kuwafichua
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Natangaza kwenye vyombo, nainadia dunia
Watafunao kimombo, bado hamjasikia?
Suluhu ya haya mambo, Amefika Masihia
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Njoo tuyapige kumbo, njoo tufanye baia
Tusiufate mkumbo, tutakuja kujutia
Mwanisikia Urambo?, Mwanza nasaha pokea
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Kama tujifanye tembo, ujumbe kuubeua
Au kuremba marembo, kwa hoja zisizofaa
Haki tutanuka shombo, wallahi na waapia
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Imekatika mitambo, wino umeniishia
Nimebakiwa na nembo, nembo ya Islamia
Nieneze kila jimbo, nitangaze Hamadia
Ni nani walioua, tuwatumie mgambo.

Mwl. Mubarak A. Nyamihasi - Mwanza

Siku ya Michezo Jamia Ahmadiyya Yafana na Kuvutia

Na Principal
Jamia Ahmadiyya Morogoro



Wanafunzi na walimu wa Jamia Ahmadiyya wakipata nasaha na maelezo juu ya lengo la michezo hiyo kutoka kwa Mkuu wa Chuo (Principal) wa Jamia Ahmadiyya, Sheikh Abid Mahmood

Kwa mara ya kwanza katika historia yake, chuo cha waalimu wa jumuiya (JAMIA AHMADIYYA) hapa nchini kiliandaa siku maalum ya michezo (sports day).

Siku hiyo maalum iliyotengwa kwa shughuli hizo ilikuwa ni Jumamosi ya tarehe 7/05/2016.

Siku hiyo michezo mbalimbali ilifanyika na washindi kupatikana. Ikumbukwe kuwa kila mwaka wanafunzi wa chuo hiki hushiriki katika mashindano mbalimbali ya kielimu na ya kimwili pia, lakini ili kuongeza hamasa zaidi mwaka huu iliamuliwa iwekwe siku maalum kwa shughuli hizo.

Siku hiyo hafla ilianza saa 2:15 asubuhi chini ya m/kiti MWL. Athuman Takato Sahib na mgeni rasmi alikuwa mkuu wa chuo sheikh ABID M. BHATTI sahib.

Hafla ilianza kwa usomaji wa Qurani tukufu iliyosomwa na ustaadh ALLY HASSAN na kisha m/kiti alimkaribisha mgeni rasmi ili atoe nasaha kwa washiriki.

Katika nasaha zake mgeni rasmi alinukuu ile hadithi maarufu ya mtume mtukufu s.a.w isemayo "Mwaminio mwenye nguvu ni bora kuliko aliye dhaifu," kisha akasema michezo husaidia kujenga na kuimarisha afya za washiriki hivyo ni vizuri kuitumia fursa hii kwa kupata manufaa.

Aliendelea kusema kuwa hadithi hiyo ya Mtume Mtukufu s.a.w inaweza kutafsiriwa kwa namna mbalimbali, la muhimu ni kufahamu kuwa pamoja na kupata burudani na kujenga afya zetu lakini pia tunapata thawabu, kwani tutakuwa tumetekeleza agizo la Mtume wetu s.a.w. Zaidi ya hayo mgeni rasmi alihimiza suala zima la kuzingatia nidhamu katika michezo na akasisitiza pia mchezo wa kiungwana-Fair play.

Baada ya nasaha hizo chache, mgeni rasmi aliongoza maombi ya kimya kisha akafungua rasmi mashindano hayo.

Shindano la kwanza lilikuwa ni fainali ya mpira wa wavu-Volley ball. Fainali hiyo ilizikutanisha timu za Shujaat na Shafqat, ambapo timu ya Shujaat ilichukua ubingwa kwa kuwabwaga wenzao wa Shafqat kwa seti 2-0.

Kisha ilifuata fainali ya mchezo wa kuruka chini-Long jump. Katika fainali hii mshindi wa kwanza alikuwa MZEE M. MZEE na wa pili alikuwa SADAM RAJAB na mshindi wa tatu alikuwa ni IDDI HASSAN.

Baada ya hapo lilifuata shindano la kupimana nguvu (kusukumana) kwa kusimamia mguu mmoja. Katika shindano hili BASHIRDIN S. MASUMBUKO alichukua nafasi ya kwanza, nafasi ya pili ilichukuliwa na MAHMOUD DIEGA na nafasi ya tatu ilichukuliwa na SAADAT MUKOYA.

Shindano hilo kwa upande wa wanafunzi wa hifdh class mshindi wa kwanza alikuwa ni A B D U R R A H M A A N RAMADHAN, wa pili alikuwa ni ZAIDUN JUMA na wa tatu alikuwa ni MASROOR FADHIL. Baada ya hapo kulikuwa na mapumziko, chakula cha mchana na sala ya Adhuhuri na Alasiri. Awamu ya pili ilianza saa 9:00 alasiri na shindano la kwanza katika awamu hii lilikuwa ni fainali ya kuvuta kamba, fainali hiyo ilizikutanisha tena timu za Shafqat na Shujaat ambapo timu ya Shafqat iliibuka mshindi wa kwanza.

Kisha lilifuata shindano la kukalia kiti kwa upande wa staff (waalimu na masheikh). Katika Shindano hili MAULANA SHEIKH AHMAD DAUD Sahib aliibuka mshindi wa kwanza akifuatiwa na MWL. MUSTAFA MAMBO Sahib katika nafasi ya pili na wa tatu alikuwa ni SHEIKH AZIZ A. SHAHZAD Sahib.

Baada ya shindano hilo, lilifuata shindano la kuruka kichurachura, ambapo mshindi wa kwanza alikuwa ni HAMZA HASSAN, mshindi wa pili ni ASHRAF RASHID na mshindi wa tatu ni ZUHEIR SAIDI.



Baadhi ya Wanafunzi wa Jamia Ahmadiyya wakiendelea na mchezo wa mpira wa wavu (Volleyball) huku wengine wakifurahia kutazama mchezo huo



Mchezo wa Mpira wa miguu (kama ulivyo umaarufu wake) ulikuwa ni miongoni mw a michezo ambayo Wanafunzi wa Jamia walishiriki kwenye mashindano hayo

Shindano la mwisho lilikuwa mpira wa miguu-al-maarufu soka. Fainali ilizikutanisha timu za Amaanat na Shujaat na matokeo ni kuwa timu ya Amaanat iliibuka bingwa baada ya kuwabugiza bila huruma ndugu zao wa Shujaat kwa mabao 5-0.

Ikumbukwe kuwa kabla ya siku hiyo, tayari yalishafanyika mashindano ya mpira wa meza (Table tennis), kupimana nguvu za mikono, mbio za miguu mitatu, riadha mita 100 na mita 1200 nk.

Mwisho mgeni rasmi aliwashukuru washiriki wote na kuwapongeza washindi na kuwataka walioshindwa kujiandaa vizuri na kuongeza bidii katika mashindano yajayo.

Mwisho.

Mwelewe Dhulqarnain

Na Al-Ustadh Ally Suleiman Magana – Tanga.

Kabla ya yote ni chukue nafasi hii kumshukuru Allah Dhul Jalaal aliyeniwezesha kukamata kalamu hii nikiwa mwenye afya njema. Alhamdulillah. Katika makala hii tutajadili masuala mazima yanayomhusu 'Dhulqarnain'. Bila shaka hili nalo ni suala kubwa linalosumbua katika jamii hususani Waislam, kwani juu ya suala hili kumekuwa na dhana mbalimbali. Kwa hakika wengi wamepotezwa katika hili.

Katika Qur'an Tukufu Suratul Kahf (18:84-89) Allah Ametueleza habari za (Mfalme) fulani wa zamani kabla ya Mtume Muhammad (saw) ambaye Allah Amemtaja kwa jina la Kiistaara, ambalo ni 'DHUL QARNAIN'. Na kwa mujibu wa Qur'an Tukufu Mfalme huyo ameonekana kuwa alieneza utawala wake sehemu za Magharibi, Mashariki n.k hii ni kwa mujibu wa aya za 87, 91 na 94 zisemazo:-

- Hata alipofika machweo ya jua
- Hata alipofika mawiyo ya jua
- Hata alipofika katikati

Pia Qur'an Tukufu yatuonesha kuwa Mfalme huyo alikuwa ni mwema na muadilifu wa hali ya juu sana kwani pamoja na kuyashinda makabila na mataifa mbalimbali lakini aliendelea kuwafanyia wema wale waliokuwa chini ya utawala wake. Hayo yanathibitishwa na aya za 88 – 89 zisemazo: "Akasema; amma anayedhulumu basi bila shaka tutamwadhibu kisha atarudishwa kwa Mola wake naye atamwadhibu adhabu mbaya. Wa amma mwenye kuamini na kufanya vitendo vizuri, basi atapata ujira mwema, nasi tutamwambia lililo rahisi katika amri yetu".

Na ama kuhusu wema kwa wale waliokuwa chini ya utawala wake tunasoma katika aya za 95 – 97 zisemazo kuwa wafuasi wake walimuomba awajengee ngome ili kuwakinga dhidi ya adui zao "YAAJUUJA WA MAJUUJA" naye alifanya hivyo na kuwataka wafuasi wake kuchangia nguvu zao kidogo tu. Na huu ndio utaratibu unaoendelea hata sasa, kwani kama watu wa sehemu fulani wana hitaji hospitali ili iwe kinga kwao dhidi ya adui maradhi, basi hapo serikali huwataka watu wa sehemu hiyo kuchangia nguvu zao ili kurahisisha kazi hiyo.

Kwa kuwa Qur'an Tukufu siyo kitabu cha hadithi za kale na vichekesho vya kila namna, basi kila jambo lililoelezwa humo linahitaji kufikiriwa kwa kina na uangalifu mkubwa, na hili la "DHUL QARNAIN" ni mojawapo miongoni mwa mambo mengi yaliyoelezwa na Qur'an Tukufu habari za DHUL QARNAIN na hekima ya kuwepo kwake ndani ya Qur'an Tukufu kama nilivyosema hapo kabla kwamba DHULQARNAIN ni jina la Kiistaara yaani siyo jina maalumu la mtu au mfalme fulani pekee; bali jina hilo aweza kupewa mtawala, Mfalme au Kiongozi yeyote ambaye sifa zake zinakubaliana na tafsiri nzuri ya jina hilo.

Maneno "DHUL QARNAIN" yanatokana na neno "QARNA" ambalo maana yake ni Karne, Cheo, Kipindi au Muhula, pembe n.k Hivyo maneno "DHUL QARNAIN" maana yake itakuwa Mwenye Karne mbili yaani mtu aliyepata kuishi katika Karne mbili. Mwenye vyeo viwili, mwenye pembe mbili, m wenye vipindi viwili n.k kwa kuzingatia maana hizo, basi ndipo twaweza kutambua Mfalme huyo alikuwa ni nani.

Tukiangalia Biblia kitabu cha EZRA 1:1-2 tunasoma; "Ikawa katika mwaka wa kwanza wa KORESH, Mfalme wa AJEMI ili kwamba neno la Bwana alilosema kwa kinywa cha YEREMIA lipate kutimizwa; Bwana akamuamsha Roho yake KORESH mfalme wa AJEMI, asema hivi Bwana Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote za dunia na ameniagiza nimjengee nyumba katika YERUSALEM uliko YUDA"

Na katika DANIEL 8:19-20 tunasoma kuwa; "Akaniambia kuwa tazama nitakakujulisha yafuatayo kuwa siku ya mwisho wa ghadhabu maana ni ya wakati wa mwisho ulioamriwa, yule kondoo mwema uliyemuona mwenye pembe mbili, hizo ndizo wafalme wa UMED na UAJEMI". Pia katika kitabu cha ISAYA 45:1-3) imeandikwa; Haya ndiyo Bwana amwambiayo KORESH, Masihi wake ambaye nimemshika mkono wake wa kuume ili kutiisha mataifa yote mbele yake ..... Nami nitakupa hazina za giza na mali zilizo fichwa mahali pa siri"

Hivyo basi kwa mujibu wa aya hizo za Biblia hapo juu zaonyesha wazi kuwa sifa za jina "DHUL QARNAIN" zinamuangukia Mfalme KORESH au CYRUS aliyekuwa mtawala wa UAJEMI ambaye pia inaaminiwa kuwa ndiye alikuwa muanzilishi wa taifa hilo la AJEMI na kihistoria yasemwa hivyo kuwa "CYRUS is the founder of the MED PERSIA EMPIRE" hii imo katika (Jewish Encyclopaedia).

Kwa kuwa m aana mojawapo ya maneno DHUL QARNAIN ni mwenye pembe mbili, hii pia inakubaliwa na Biblia katika Daniel 8:20 ambapo hapo Daniel alikuwa akiona maono au kashf. Pia maana nyingine ya Dhulqarnain ni Mwenye vyeo viwili na hii pia yakubaliwa na Biblia, kwani KORESH anaonekana alikuwa na vyeo viwili navyo ni Ufalme kama ilivyoandikwa katika EZRA 1:1-2 pia aliitwa Masihi katika ISAYA 45:1-3. Hivyo ni vyeo viwili sawa kabisa na m aana ya maneno "DHUL QARNAIN"

Katika sura hiyo ya 18:85 Allah anasema kuwa; "Bila shaka tulimuimarisha katika ardhi, na tukampa njia za kupatia kila kitu" Neno lililotumika katika aya hiyo ni "SABABAN" ni neno ambalo pia maana yake ni sababu ya kupata kitu fulani ambacho ni muhimu sana. "Hata alipofika machweo ya jua akaliona linatua katika chemi chem iliyovurugika" (18:87). Hii inaonesha kuwa Mfalme CYRUS alifika Magharibi kwenye Bahari nyeusi (Black sea), Kaskazini Magharibi ya AJEMI (IRAN), kwani jua linapozama mtu akiwa Pwani hiyo huliona kama limezama katika matope, hii ni kutokana na maji ya Bahari hiyo kuwa meiusi. Neno 'Ainu' yaani chemichem linalopatikana katika aya hiyo, maana yake pia ni "Mtazamo" hivyo hii inaonesha kwamba Mfalme CYRUS aliamini Maisha baada ya kifo, kwani inaaminika kuwa yeye alikuwa mfuasi muaminifu wa dini ya ZOROSTA.

Katika aya za 88-89 yaonekana kuwa waliomkataa Mfalme CYRUS waliadhibiwa nao walioamini walipata malipo mema. Hii inaonesha kuwa Mfalme DHULQARNAIN alikuwa ni fundi na mbunifu wa kupanga taratibu madhubuti katika utawala wake. "Hata alipofika mawinyo ya jua akaliona linawatokea watu tusiowawekea pazia la kuwakinga nalo18:91 maneno yanayoonesha kuwa Mfalme DHUL QARNAIN (CYRUS) alifika sehemu ya Mashariki ya AJEMI na sehemu hiyo hupata Kiangazi kwa muda mrefu katika mwaka. Na pia inaonesha jinsi Mfalme huyo alivyoeneza utawala wake, aliufikisha sehemu za AFGHANSTAN, BRUSHTAN, SAISTAN, MESHEK na DUSHARAN.

Katika aya ya 92 Mwenyezi Mungu anasema; "Na tulikuwa tumezunguuka habari zilizokuwa pamoja naye". Hii yaonesha kuwa habari zake hizo huyo DHUL QARNAIN zitadumu na hiyo inathibitishwa kwa habari hizo kurekodiwa katika Qur'an Tukufu jinsi vile inavyodumu ndivyo habari zake DHUL QARNAIN zitakavyodumu.

Katika aya ya 94 Allah anasema; "Hata alipofika kati kati ya milima miwili akakuta watu nyuma yao ambao waliweza kwa shida kufahamu neno" aya hii yaonesha kwamba Mfalme CYRUS alifika sehemu ya milima ya KAUKASIAN kwenye Bahari ya KASPIAN, na inaonesha watu aliowakuta huko lugha yao ilikuwa tofauti na lugha ya Mfalme huyo CYRUS.

Katika aya ya 95 inaonesha kuwa aliowakuta nyuma ya mlima au kati kati ya mlima walimuomba msaada Mfalme CYRUS awajengee ngome au ukuta ili kuwakinga dhidi ya mashambulio ya YAAJUUJA WA MAJUUJA. Hii yaonesha kuwa watu hao walijificha huko ili wasishambuliwe na hayo YAAJUJA WA MAJUUJA. Neno YAAJUUJA WA MAAJUUJA chimbuko lake ni AJIIJ ambalo maana yake ni "Ulimi wa moto" na neno moto limetumika katika Qur'an Tukufu Sura 5:65 kwa maana ya vita. Hivyo watu waliokaa kati kati ya mlima walifanya hivyo ili kujikinga na mashambulizi ya kivita yaliyoelekezwa kwao. Hii pia inasadikisha kuwa YAAJUUJA WA MAAJUUJA hawakuwa WARUMI kwani inasadikika Mfalme CYRUS alikuwa ni MUIRAN. Katika aya ya 97 ya sura hiyo Kahf, inaonesha kuwa Mfalme CYRUS alijenga ukuta kwa kutumia chuma na shaba iliyoyeyushwa, vitu hivyo hufanya ukuta kuwa mgumu sana. Hayo yanathibitishwa na aya ya 98 inayoonesha kuwa YAAJUUJA WA MAAJUUJA hawakuweza kuukwea wala kuutoboa ukuta huo. Pia ina aminika kuwa watu hao walikuwa wafanyabiashara waliokuwa matajiri wakubwa sana. Kihistoria ukuta huo una urefu wa futi 29 na upana wa futi 10 na ulikuwa na minara ya saa nao ulikuwa katikati ya URUS na IRAN ambapo hivi sasa sehemu hiyo inaonekana ipo upande wa URUS.

Katika aya ya 99 Mwenyezi Mungu anasema; "Akasema (Dhul Qarnain) hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu". Hii inaoneshwa jinsi Mfalme CYRUS alivyokuwa mcha Mungu wa hali ya juu. Pia maneno ya mbele katika aya hiyo yanaonesha kuwa, zama zitafika ambapo YAAJUUJA WA MAAJUUJA watavuka ukuta huo kwa kupitia juu – angani, na hii ndio sifa mahsusi ya hao YAAJUUJA WA MAAJUUJA kama inavyothibitishwa na Qur'an Tukufu sura 21:97; "Hata atakapofunguliwa YAAJUUJA WA MAAJUUJA nao toka kila mahali pa juu watakuja mbio".

Hii inaonesha kuwa hao YAAJUUJA WA MAAJUUJA watakapokuwa na nguvu kiasi hicho juu ya anga dunia yote itakusanywa pamoja na hii inathibitishwa katika sura 21:5. Kwa kuwa Qur'an Tukufu si kitabu cha hadithi za alinacha na vinginevyo, bali tunaamini kuwa kila kitu kilichoelezwa ndani yake aidha onyo, agizo au bishara (Tabiri), kwa sababu hiyo basi na sisi hatuchukulii habari hii kuwa kama historia tu, bali tunaamini kwamba hapa Qur'an Tukufu inaashiria juu ya ufikaji wa MUJADID wa zama za mwisho, aliyetegemewa katika hii dunia. Na kwa kuwa suala la kuja kwa IMAM MAHD ni jambo ambalo kubwa mno, hivyo Allah Amelieleza jambo hili kwa hekima ya hali ya juu sana ili lieleweke vyema na wanadamu hususan Waislam. Na vitabu mashuhuri vya Kiislam vinamueleza Mujadid huyo kama ni "MASIHI na MAHD"

Kwa kuwa sura nzima ya AL-KAHF ina madhumuni kuu nne ambazo ni:-

1. As –Haabul Kahf
2. Kisa cha watu wawili
3. Israa ya Nabii Mussa na
4. Habari za Dhul-Qarnain.

Nasi hapa tunajadili habari za Dhul-Qarnain hivyo hapa ikumbukwe tu kwamba habari hizi za Dhulqarnain zimekuja baada ya Israa ya Nabii Musa (as) basi hii ni kwa sababu katika Israa ya Nabii Musa (as) kuna utabiri wa kufika yule aliye Mfalme wa Manabii yaani Mtume (saw), na katika maudhui hii ya Dhul qarnain kama nilivyoeleza hapo nyuma kuwa ni utabiri wa kufika kwa IMAM MAHD ambaye ni mtoto wa kiroho wa Mtume (saw) na ambaye alitakiwa kuwa msaidizi mkuu wa Mtume (saw) hasa katika zama za mwisho ambapo Waislam wataacha kabisa mafundisho mema na mazuri ya dini tukufu ya Islam, kama ilivyothibitishwa hali hiyo na Qur'an Tukufu sura 25:31; "Na Mtume atasema; Ee Mola wangu, hakika watu wangu wameifanya Qur'an Tukufu hii kuwa kitu kilichoachwa"

Hali kadhalika Mtume (saw) aliieleza hali hiyo, pale aliposema; "Kutoka kwa Ally ra. Amesema Mtume saw amesema kuwa zitafika zama ambapo Uislam hautabakia isipokuwa jina ....." hivyo kutokana na hali mbaya kama hiyo kuwakumba Waislam ndipo Allah Atamtuma Imam Mahd kuja kuwaredhesha Waislamu katika Uiuslam sahihi na hii inathibitishwa na kauli ya Mtume (saw) pale aliposema; "Imesimuliwa na Abuu Huraira ra amesema kuwa; tulikuwa tumekaa na Mtume (saw) ndipo ikateremshwa kwa Mtume (saw) Surat Jumaa na ndani yake ilikuwa aya isemayo; "Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao". Abuu Huraira amesema kwamba nilisema, ni nani hao ewe Mjumbe wa allah? Naye Mtume (saw) hakujibu mpaka nilipomuuliza kwa mara ya tatu, na kati yetu alikuwapo SALMAN FAARIS basi Mtume (saw) akaweka mkono wake juu ya bega la Salman Faaris kisha akasema; ijapokuwa imani itatundikwa kwenye nyota ya Kilimia, wataifikia watu miongoni mwa hawa au mtu miongoni mwa hawa (Bukhar Kitabu Tafsir Suratil Jumaa).

Hali kadhalika pia katika Muslim imeelezwa katika maneno ya mwisho ya hadithi hiyo kuwa; "Japokuwa dini itatoweka na kutundikwa kwenye nyota ya kilimia mtu miongoni mwa wa Faaris ataiondoa (huko na kuirejesha duniani) au amesema Mtume (saw) mtu miongoni mwa watoto au uzao wa kifaris mpaka ataifikia. (MUSLIM BAAB FADHIL FAARIS).

Bila shaka msomaji mpaka hapa kwa dalili hizo tumekwisha fahamu na tumeona kwamba Imam Mahd alitarajiwa kudhihiri wakati ambapo Waislamu watakaposahau na kuacha kabisa mafundisho ya dini yao yaliyomo katika kitabu cha Allah. Juu ya hili msomaji hebu kwanza tuangalie hadithi iliyopokelewa na Bi. Aisha (ra) isemayo; "Kutoka kwa Bi. Aisha, mtu mmoja alimuuliza Mtume (saw) ni watu gani ambao ni bora? Mtume (saw) akasema; ni wale ambao wapo katika karne ambayo mimi mwenyewe nipo ndani yake, kisha watu wa karne ya pili, kisha watu wa karne ya tatu" (Muslim).

Kisha tuangalie aya hii ya kitabu Tukufu isemayo; "Allah hulitengeneza au hulipanga jambo toka mbinguni mpaka ardhini, kisha linapanda kwake siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu moja mnayotumia katika hesabu" (32:6).

Neno "Amr" – jambo, muradi wake hapa ni Qur'an Tukufu. Hivyo basi sawa na hadithi hiyo hapo juu inaonesha kuwa karne tatu za kwanza yaani

Endelea uk. 9

Mwelewe Dhulqarnain

Kutoka uk. 8

tangu wakati wa Mtume (saw) na baada yake, zitakuwa ni bora na kheri kwa Waislam. Lakini baada ya hapo aya hiyo hapo juu yaonesha kuwa zitafuata karne kumi ambazo sheria ya Qur'an Tukufu itaonekana kama vile imepaa kwenda mbinguni na kufika kwenye nyota ya kilimia. Hivyo basi hapa kuna karne kumi na tatu (13), kwa hiyo basi Imam Mahdi alitazamiwa kufika katika karne ya kumi na tatu, kumi na nne.

Na Mtume (saw) alituhakikishia juu ya ufikaji wa Imam Mahd katika hadithi iliyopokelewa na Annas (ra); "Annas (ra) amesema kuwa nilimsikia Mtume (saw) akisema, kiyama hakitafika mpaka Allah ainue kundi litakalotokea HINDI nalo litakuwa pamoja na Imam Mahd ambaye jina lake ataitwa AHMAD (Annajmu Thaaqib Juzuu 2 uk.41-42)

Mpaka hapa msomaji tunaona Mtume (saw) ametubainishia wazi jina la Imam Mahd kuwa ataitwa Ahmad na hata sehemu atakayoshukia kuwa ni Mashariki ya Dunia INDIA; basi kwa kauli hiyo ya Mtume (saw) KADIAN ndio INDIA huko mashariki ya DAMASCAS na ni mashariki ya dunia ndipo atakapomshushia ili kufikisha ujumbe wa Allah naye huyo si mwingine bali ndiye Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad ambaye ndiye mwanzilishi wa Jumuiyya hii ya Waislam wa Ahmadiyy ulimwenguni na sifa zote za DHUL QARNAIN dhahiri shahiri zinaangukia kwake, naye ndiye Dhulqarnain wa zama zetu hizi.

Bila shaka msomaji aweza kuuliza au kupata shaka kwamba kuna mlingano gani kati ya Dhul qarnain wa kwanza ambaye ni Mfalme wa Ajemi (CYRUS) na Dhulqarnain wa zama hizi (MIRZA GHULAM AHMAD) aliye mwanzilishi wa Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Basi ni vizuri sasa tuangalie sifa za Dhul qarnain wa kwanza kama zilivyoelezwa katika Qur'an Tukufu sura hiyo AL-KAHF na kisha tulinganishe pamoja na kauli ya Mtume (saw) kumhusu Imam Mahd. Pia kuna Mawalii na Wacha Mungu mbalimbali wa zamani ambao wanakubaliana kuwa kauli hiyo ya Mtume (saw) kuhusu jina la Imam Mahd ataitwa Ahmad. Basi sasa na tuanze kuangalia kauli za Mawalii hao na Wacha Mungu hapa nitawataja Mawalii wawili;

1. Kwanza kabisa ni Walii mkubwa aitwae SHAH NEEMATULLAH aliyezaliwa zaidi ya miaka 819 iliyopita. HADHRAT SHAH NEEMATULLAH ambaye aliishi katika mwaka 560 A.H katika Kaswida yake maarufu iliyokuwa katika lugh ya kiajemi inayojulikana sana miongoni mwa Waislam hususan wa huko Hindi, walii huyo amesema; "Nitakayo tabiri siyo kuwa njia ya nyota, bali nimefahamishwa na Allah, yatatokea baadae. Naona maajabu yakitokea baada ya mwaka 1200 A.H watu watapotea na roho zao zitapotea. Dhuluma itaenea kila mahali duniani. Naona vita na machafuko kutokea huku na huko. Mapinduzi yatatokea yatakayowafanya mabwana kuwa watumishi na watumishi kuwa mabwana, na sarafu mpya itatumika nchini humu, njaa itaenea na mabustani hayatazaa matunda. Lakini msitikisike wala msihangaike. Kwani furaha ya kuungana na Mola imekadiriwa kupatikana katika zama hizo. Msimu huo ndipo jua la msimu wa kusi na rutuba ukishapita, maua yatachanua na jua litachomoza. Jina la huyo jua nalisoma ni AHMAD nami naona umashuhuri wake kuenea kila mahala. Mheshimiwa ndilo jina lake ninalosoma na mwanaye namuona ni mashuhuri".

2. Walii mwingine aliyesadikisha jina la Imam Mahd kuwa ni AHMAD ni IMAM YAHYA BIN AQIB aliyeishi katika karne ya 5 A.H yeye amewahi kueleza juu ya zama zetu hizi, katika shairi lake la lugha ya Kiarabu lililoandikwa katika kitabu kiitwacho SHAMSUL MAARIFAL KUBRA uk.340 yeye amesema kuwa; "Mimi nimefumbua siri za maajabu yatakayotokea baadae. Nyota moja kubwa itaonekana na siku za wazungu kutawala Pwani na milimani. Hii bila shaka itakuwa alama ya kudhihiri kwa Imam Mahd na baada ya Mahd atadhihiri 'Mahmood' ambaye atamiliki nchi ya 'SHAM' bila ya kupigana vita. Yeye atadumu kutoa mali yake katika kila hali (ili kuuhami Uislam)".

Basi hizo ni kauli za Mawalii wakieleza jina la Imam Mahd na zama za kudhihiri kwake.

Sasa na tugeukie katika Furqaani nayo pia tuone. Kwa mujibu wa aya ya 84 na nyinginezo ambazo neno DHUL QARNAIN linapatikana, na kwa kuwa maana mojawapo ya maneno hayo ni "Mwenye karne mbili". Yaani mtu atakayeishi katika karne mbili. Na inasadikiwa kuwa Mfalme CYRUS aliishi katika karne mbili, kati ya mwaka 449 – 568 B.C yaani 4 – 5 B.C. na ndivyo hivyo hata Seyyidna Ahmad (as) naye aliishi katika karne mbili tofauti, kwani alizaliwa tarehe 13/02/1835 – 26/05/1908 hii inaonesha kuwa aliishi kati ya karne ya 19 na 20 A.D, bali hata kwa kiarabu pia inaonesha kuwa Seyyidna Ahmad (as) aliishi kati ya karne ya 14 na 15 A.H Huu ndio mlingano mkubwa kabisa uliyopo na ulio sawa na maana ya jina lenyewe. Pia maana nyingine ya DHUL QARNAIN ni Mwenye vyeo viwili. Mfalme CYRUS alikuwa na vyeo vieili kama tulivyoona katika EZRA 1:1-2 ambapo imesema alikuwa Mfalme wa Ajemi na pia Mfalme huyo alikuwa ni Masihi kama tulivyoona katika ISAYA 45:1. NA HIVYO NDIVYO ALIVYOKUWA Seyyidna Ahmad (as) kwani yeye ndiye Masihi na Imam Mahd. Katika aya ya 85 Allah anasema; "Hakika tumemuimarisha katika ardhi na tumempa njia ya kupata kila kitu". Neno lililotumika katika aya hiyo ni sababu ya kupata kitu. Hivyo hii inaonesha kwamba Mfalme CYRUS alikuwa na maarifa ya kiutawala na kupata mafanikio katika uongozi wake. Na vivyo hivyo ndivyo alivyokuwa Seyyidna Ahmad (as) kwani alipewa kutoka kwa Allah maarifa, hekima ya hali ya juu na elimu ya kutosha ya Qur'an Tukufu ili kuwaongoza Waislam, na Allah anasema; "Allah Humpa hekima amtakaye na aliyepewa hekima bila shaka amepewa heri nyingi".

Pia katika ISAYA 45:3 Imesemwa; "Nami nitakupa hazina za giza na mali zilizofichwa mahali pa siri". Historia ya Seyyidna Ahmad (as) inathibitisha jambo hilo. Bali yeye mwenyewe alipata kusema katika ubeti mmoja wa shairi lake kuwa; "Nimepewa kutoka kwa Mola wangu elimu ya wazi na ninajua yale msiyoyajua". Katika aya ya 86 Allah amesema; "Ndipo akafuata njia". Basi hii inaonesha kuwa Mfalme CYRUS baada ya kuona ishara za Allah alishika desturi ya kumtumikia Allah. Hayo yanathibitishwa katika EZRA 1:2 Pale alipojenga nyumba ya ibada. Naye pia Seyyidna Ahmad (as) alifuata njia iliyo bora aidi, nayo ni kupigania Uislamu kwa hali na mali.

Katika aya ya 87 inaonesha DHUL QARNAIN wa kwanza alifika sehemu ambapo jua alililona linazama katika matope. Kwa DHUL QARNAIN wa zama zetu yaani Seyyidna Ahmad (as) hii inaonesha kwamba; kwa kuwa kawaida ya jua huzama upande wa Magharibi, basi maana yake ni kuwa zama za kufika Imam Mahd atakuta watu wa Ulaya Magharibi wakiwa wanayadharau mafundisho ya Kiislam kwa kuyatupia masingizio ya kila namna hivyo kuyapaka matope yasieleweke vizuri kwa watu watafutao ukweli.

Hivyo basi Imam Mahd kazi kubwa atakayofanya ni kuwaita watu wa Magharibi kwenye mafundisho ya Islam na kuwadhihirishia ubora wa mafundisho hayo. Kwa hekima ya juu sana ambapo hatimaye watayaelewa vema na kuyakubali.

Historia ya Jumuiyya na kuwepo kwake katika nchi za Magharibi na Amerika ni ushahidi wa hayo yote. Tena kisha Allah amesema; "Tukasema ewe Dhul qarnain uwaadhibu au uwafanyie wema ..... mwenye kuamini na kufanya vitendo vizuri atapata ujira mwema" (88-89). Hii inaonesha kwamba baada ya kudhihiri kwa Imam Mahd na kujieleza wazi kwa njia ya hoja na dalili na kila kitu kubainika wazi, basi watakao mkataa wataadhibiwa. Na hii ilitokea wakati wa Seyyidna ahmad (as) kwani wale waliokuwa wapinzani wake waliadhibiwa kwa ugonjwa wa Tauni. Hiyo ilikuwa mwaka 1903. Katika aya 91-94 zinaonesha kwamba Dhul qarnain alifika mawio ya jua na huko aliwakuta watu waliochomwa na jua na walikuwa wagumu wa kuelewa. Ibara hii kwa Imam Mahd wa zama hizi inaonesha kwamba atakapofika, basi atawakuta watu wa Ulaya Mashariki (URUSI) wakiwa hawana habari juu ya mafundisho ya Kiislamu, na hivyo basi jua la mwanga wa Islam halitakuwa na faida yoyote kwao. Hivyo Imam Mahd atafanya kazi kubwa ya kuwaelimisha ubora na umuhimu wa mafundisho ya Islamu na hekima yake. Pamoja na ugumu wao lakini kwa juhudi kubwa na hekima ya Imam Mahd wtayaelewa ubora na umuhimu wake na baada ya kuyaelewa watajiunga na Jumuiyya, nao watatoa michango mikubwa katika kueneza ujumbe wa Imam Mahd na Islam kiujumla duniani kote. Juu ya jambo hili historia inakubali kabisa, kwani watu wa Urusi hawakuelewa kabisa mafundisho ya Islam bali walikanusha hata kuwepo kwa Mungu.

Lakini kwa busara na hekima za Imam Mahd aliwafikishia mafundisho ya Kiislam nao waliyakubali na wanaendelea kujiunga na Jumuiyya kwa wingi sana, nao wanajitolea michango yao kwa kuenea ujumbe wa Imam Mahd na Uuislam kwa jumla.

Katika aya 95 -98 inaonekana kuwa Dhul qarnain aliombwa na wafuasi wake awajengee ukuta ili kuwakinga dhidi ya maadui zao. Hii yaonesha kuwa zama za kufika Imam Mahd atawakuta Waislam wakubwa wamekata tamaa juu ya dini yao, nao hawatakuwa na elimu ya Uislam, jambo litakalosababisha Imani kutoweka miongoni mwao kama vile ndege arukavyo kutoka katika kiota chake. Na kwa kuona hivyo maadui wa Islam watashambulia mafundisho ya Uislam na Mtume wake (saw) kwa hila za kila namna na huku wakijaribu kutumia hata baadhi ya aya za Qur'an Tukufu ili kuwanyamazisha kabisa Waislam. Basi pindi atakapofika Imam Mahd Waislam wachache watakaokuwa na busara kidogo miongoni mwao hawataacha kuomba msaad kwa Imam Mahd ili kuwasaidia kuwakinga kutokana na mashambulizi ya maadui zao. Na hii ilitokea mwishoni mwa mwaka 1896 pale Waislam wote walipokubali kwa kauli moja kumteua Seyyidna Ahmad kuwa msemaji mkuu kwa upande wa dini ya Kiislam katika mkutano wa dini zote uliioitishwa mnamo tarehe 26/12/1896 ili kujibu maswali matano kutoka kwa Bw. Mmoja aliyeitwa SWAMI SHUGHAN CHAND, naye Seyyidna Ahmad (as) alikubali mara moja wito huo na kuutetea Uislam kikamilifu kwa kutumia ushuhuda madhubuti wa Qur'an Tukufu na hivyo kupelekea hotuba yake kuibuka mshindi dhidi ya hotuba zote zilizotolewa kwenye mkutano huo. Na hivyo kuzima kabisa kabisa mashambulizi ya maadui dhidi ya Uislam, kwani siku ile Uislam umeonekana kuwa ni dini ya pekee iliyo hai na iliyobora na yenye mafundisho mazuri kuliko dini nyingine yoyote na hivyo kutimia maneno ya Mtume (saw) yasemayo; "YAKSIRU SWALIBA WA YAQTULUL KHIN-ZIIR" Yaani atavunja msalaba na ataua nguruwe. Bali hiyo pia inatimia hata kwa wafuasi wa Imam Mahd. Kwa mfnao Maulana Sheikh Jalaluddin Shams alipotoa darasa la Qur'an Tukufu huko Misri, mara baada ya darasa hilo aliombwa na wakazi wa hapo kwamba akae hapo ili awaelimishe zaidi dini ya Kiislam. Pia hiyo ilitokea kwa Khalifa wake wa pili Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad pale alipotoa darasa kule Madina, na baada ya darasa hilo wenyeji wa Madina walimuomba aendelee kubakia nao hapo ili kuwaelimisha vya kutosha juu ya Uislamu, lakini kwa hekima kubwa aliwajibu kuwa – Uislamu umeshahama hapo na kwenda sehemu ya mbali – Mashariki hivyo nao hawana budi kuacha kiburi na kuufuata Uislamu huko uliko. Na pia hapa kwetu Tanzania hali hiyo ilitokea pale Maulana Sheikh Jamil Rahman Rafiq alipoombwa na hata Waislamu wa Sunni ili atoe majibu ya kitabu cha "WANA WA IBRAHIMU" kilichokuwa kimetungwa na PADRI H.P ANGLAS ambacho ndani yake mashambulizi ya kikatili dhidi ya Uislam na Mtume (saw) yalifanywa. Nao waliahidi kuwa kama Sheikh atatunga kitabu kumjibu Padre huyo basi wao watatoa mchango ili kukichapisha na kukieneza kitabu hicho. Ndipo Maulana Sheikh Jamil Rahman Rafiq alipokubali ombi hilo kwa mikono miwili na kutunga kitabu ili kumjibu Padri huyo. Kitabu hicho cha majibu alikiita kwa jina la "MWANA MKUU WA IBRAHIMU" ambamo ndani yake majibu mazuri yenye hoja na dalili za wazi yalitolewa. Na hivyo kumnyamazisha Padri huyo na wale wote waliokuwa na mawazo kama yake.

Hivyo basi ama kuhusu ukuta uliojengwa na Dhul qarnain wa zama hizi ambaye ndiye Imam Mahd ni hii Jumuiyya ya Ahmadiyya na hoja zilizojaa elimu ya hali ya juu ya kiroho na kiucha Mungu. Ambapo hakuna mtu yeyote ambaye ni adui awe Mwislam au asiwe Muislam atakayeweza kuvunja hoja za elimu ya Imam Mahd na wafuasi wake kwa ujumla. Katika aya ya 99 ya sura h iyo inaonekana kwamba Dhul qarnain baada ya kujenga ukuta akasema; "Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu". Hii inaonesha jinsi Dhul qarnain alivyokuwa mnyenyekevu mbele ya Muumba wake. Hii pia inaashiria kuwa Imam Mahd atakuwa mtiifu mbele ya Allah na pia atakuwa mcha Mungu wa hali ya juu.

Katika DANIEL 8:20 ambapo Daniel alikuwa akioneshwa kashf kuhusu zama za mwisho, alioneshwa kwa sura ya kondoo, katika kitabu cha tafsiri za ndoto ATA-TWIIRUL –ANAAM imeandikwa kwamba, yule anayeona kondoo katika njozi, basi hiyo inaashiria kuwa mtu mcha Mungu. Hivyo ndivyo alivyokuwa Seyyidna Ahmad (as). Hivyo basi Dhul qarnain wa zama hizi ndiye huyu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad – MASIHI NA IMAM MAHD na kuhusu ukuta alioujenga ndiyo hii Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya na kwa fadhila za Allah hakuna atakaye weza kuuvunja ukuta huo kwa njia yoyote. Basi ni wito kwa waitakao salama kutoka kwa Mola wao wafanye hima waje wakae katika ulinzi wa Imam wa zama hizi chini ya ukuta huo ulio imarika usiotoboka wala kutikisika kwa kugongwa na maadui.

Hiyo ndiyo mantwiki ya kisa cha Dhul qarnain iliyo sahihi na yenye hakika isiyo na shaka kabisa.

Ziara ya Amir sahib mkoani Shinyanga

Kutoka uk. 12



Jukwaa kuu wakati wa Jalsa Salana ya Mikoa ya Shinyanga na Simiyu 2016:

Amir sahib akiwa pamoja na wageni waalikwa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ofisi ya RPC Shinyanga pamoja na viongozi wa Jamaat mikoa ya Mwanza na Shinyanga

Jamaat pamoja na viongozi wa Serikali ya kijiji na Uwepo wa wanajamaat pamoja na wanakijiji wa hapo.

Aliwaasa kuwa pamoja na ufunguzi huu wa msikiti mnatakiwa muelewe umuhimu wa jambo hili, alisema sisi sote ni binaadamutupo hapa Duniani na tumejikuta tupo hapa Buchama, sasa jambo la msingi ni kwa kila mmoja wetu kujiuliza kuwa tupo hapa Duniani kwa lengo gani, je tuliletwa hapa kulima tu na kuzaana tu? La! Bali tuliumbwa na Allah Mtukufu kwa kazi maalumu ambayo ni kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Kuabudu maana yake ni kumtambua Mola wetu, tutambue Utukufu wake, tutambue sifa zake. Kwa kawaida sisi binadamu tunapotengeneza kitu tunakitengeneza ili tufikie Malengo yetu tuliyokusudia. Hivyo kila kitu tunakishughulikia kwa juhudi kubwa mpaka tufikie malengo yake. Kwahiyo Allah baada ya Kutuumba sisi hakutuacha Bure tu, bali alituwekea njia mbalimbali za kumjua na Kumwabudu Yeye. Na hivyo Allah Aliwatuma Manabii mbalimbali ili kuja kutufundisha kuwa Mwenyezi Mungu anataka nini.

Miaka 1400 iliyopita Allah Mtukufu alimtuma Mtume Muhammad s.a.w ili kuja kuwa Nabii kwa Wanaadamu wote, na Allah Akakadiria kuwa sharia yake ya Qur`an Tukufu itumike mpaka mwisho wa Dunia.

Pamoja na uzuri wa Mafundisho hayo lakini bado kulikuwa na ishara ya watu kuacha mafundisho hayo na hatimaye kurudi nyuma, hivyo sawa na Haja Allah Alimtuma Masih maud a.s ili kuja kurekebisha hali hiyo na kuturudisha kwenye mafundisho sahihi ya Dini Tukufu ya Islaam, na alipofika Masih Maud a.s ilitulazimu sawa na Amri ya Mtume s.a.w kujiunga naye ili tuweze kusalimika.

Maamuzi mliyofanya ya kujiunga na Jamaat ni maamuzi mazuri na mnatakiwa kushikamana na Jamaat hii ili musalimike. Kumbukeni kuwa baada ya kujiunga na Jamaat fahamuni kuwa mmefanya maamuzi makubwa na ni lazima muhakikishe kuwa mnafuata nidhamu kubwa.

Kumbukeni pia kuwa Msikiti huu umejengwa kwa ajili ya Ibada zenu na hivyo munalo Jukumu la kuustawisha .Tujiepushe na mambo ya fitina na siasa, tunatakiwa kuwa wamoja, mnatakiwa kujitahidi pia kuonyesha hamu ya kupata elimu hasa ya Dini.

Mwl Ame sahib alimalizi nasaha zake kwa watu wa Buchama kwa kuwaambia kuwa , Amir sahib anajali hali zetu na kutokana na Mapenzi aliyo nayo kwetu ndio maana amekuja kututembelea na kutujulia hali zetu, hivyo ni lazima nasi tuonyeshe upendo mkubwa kwa ajili ya Jamaat na Islaam kwa Ujumla.

Baada ya Nasaha hizo kutoka Kwa Mwl Ame Sahib, Amiri sahibu alituongoza katika ufunguzi huo kwa kuondoa kitambaa kilichofunika Bango la Ufunguzi na baada ya jambo Hilo yalifuatia maombi ya kimya kwa wote yaliyoongozwa na Amir Sahib. Na baada ya maombi tuliingia msikitini kwa ajili ya sala ya Adhuhuri pamoja na Alasiri. Sala hizo ziliongozwa na Amir Sahib. Baad ya sala kililetwa chakula kilichoandaliwa na wanajamaat wa Buchama kwa ajili ya sherehe hiyo ya Ufunguzi.

Msafara wa Amir Sahib uliondoka kijijini hapo saa tisa na nusu alasiri kurudi mjini kwa ajili ya kupumzika na kujiandaa kwa ajili ya safari Ya kesho yake.

ZIARA NA UFUNGUZI WA MSIKITI WA JAMAAT TAWI LA SAMUYE.

Siku ya Jumanne tar 24/05/2016, Msafara wa Amir Sahib uliingia kijijini Samuye saa saba kamili mchanan na moja kwa moja alifikia Msikitini.

Baada ya kufika Msikitini Amir Sahib alifanya Ufunguzi wa Msikiti na baada ya hapo aliongoza maombi ya kimya na baadae ilitolewa Adhana kwa ajili ya Sala ya Adhuhuri, sala ilisaliwa kwa kuongozwa na Amir Sahib, na baada ya hapo sherehe za ufunguzi zilianza kwa usomaji wa Qur`an Tukufu iliyosomwa na Mwl wa tawi la Samuye Abdulghan Msimbe. Kisha ilifuatiwa utambulisho wa viongozi mbalimbali wa Jamaat na Serikali ambap pia alikuwepo Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Samuye ambaye pia nae ni Mwanajamaat wa tawi hilo.

Baada ya utambulisho huo Amir sahib alisimama na kutoa nasaha zake kwa wanajamaat wa hapo na alianza kwa kuwakaribisha wageni waalikwa katika msikiti wetu, alisema sisi ni waislamu wa Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyyana Jamaat hii ni Jamaat ya Kimataifa kwa sababu inapatikana katika nchi 207 duniani na hatuna Shaka juu ya hilo, ila tofauti yetu na waislamu wengine ni kwamba sisi tunae Kiongozi mmoja Duniani ambaye ni Khalifa wa Zama lakini wenzetu hawana, tunajitahidi kudumisha Sala na kufanya Matendo mema na hii ndio tofauti iliyopo kati yetu na waislamu wengine.

Aidha aliwaasa wanajamaat wa Tawi la Samuye kuwa mmepata msikiti, hii ni nyumba ya Allah hivyo mnatakiwa kuistawisha kwa kufanya ibada ndani yake, mnatakiwa mjitahidi kuja Msikitini na mjitahidi kuwaleta watoto wenu kwani hapa mnae Mwalimu ambaye yupo hapa kwa ajili ya kuwafundisheni. Alisema pia kuwa sisi kama uongozi kwa upande wetu tumetimiza wajibu wetu, hivyo ni wakati wenu sasa nanyi mujitahidi kutimiza wajibu wenu, leteni watoto wenu ili waje wabadilishwe kuwa wema.

Kumbukeni pia kuwa hapa mkoani Shinyanga tuna maeneo mengi ambapo tunao ndugu zetu wengi wa kiroho ambao hawajapata msikiti wala Mwalimu wa kuwafundisha na kuwaongoza, lakini ninyi mmepata bahati hii, mmepata Msikiti, mnae Mwalimu na mmefanikiwa kupata MTA na Soler ambayo inawapatieni nishati ya umeme na mnayo fursa nzuri ya kuangalia na kumsikiliza Kiongozi wetu Mkuu Duniani (Khaifatul Masih wa Zama).

Aidha Amir sahib aliwaeleza kuwa sisi hatukuja hapa kwa ajili ya biashara wala mambo ya siasa, kama kati yenu kuna mtu anayekunywa pombe basi aache, na kama kati yenu yupo anaye fanya mambo yasiyofaa na yasiyo kubaliwa na Dini tukufu ya Islaam basi anatakiwa ayaache mara moja.

Jambo la mwisho ninalopenda kuwakumbusheni ni kuwa Jumuiya yetu inaongozwa na Kauli mbiu ya LOVE FOR ALL HATRED FOR NONE yaani Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote, ndiyo maisha na taswira halisi ya Jamaat, hivyo kila mmoja wetu anatakiwa aishi sawa na kauli hiyo. Sisi ni watu tunaotakiwa kuishi kwa unyenyekevu mno hata watu wawe mashahidi ya kwamba mmebadilika kutokana na ninyi kujiunga na Jamaat Ahmadiyya, hilo ndilo tunalolihitaji kutoka kwenu na sio mambo ya Kidunia au mengine. Nahii ndio sifa inayotakiwa muwe nayo.

Baaada ya sherehe hizo za ufunguzi kumalizika watu waliohudhuria walipata chakula kilichoandaliwa kwa ajili yao kutoka kwa wanajamaat wa Samuye. Na baadae msafara wa Amir sahib uliondoka hapo saa tisa kamili kuelekea eneo lingine ambalo alikuwa anasubiriwa kwa shughuli kama hiyo.

ZIARA NA UFUNGUZI WA MSIKITI WA JAMAAT TAWI LA NHUMBILI.

Siku ya Jumanne tar 24/05/2016 saa tisa na nusu alasir msafara wa Amir sahib na wajumbe wake walifika katika tawi hili la Nhumbili na moja kwa moja alisalimiana na wanajamaat waliojipanga katika mistari na baadae alielekea msiktini na sherehe za ufunguzi zilianza kwa usomaji wa Qur`an Tukufu pamoja na Tafsir iliyosomwa na mwanajamaat moja wa tawi la Buichama ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Msingi katika kijiji jirani na hapo, na kufuatiwa na Mwenyekiti wa kijiji ndg Waziri Kasenga ambaye yeye alitoa shukurani nyingi kwa Allah kwa kuwezesha tukio hili kubwa kufanyika hapa na aliushukuru uongozi wa Jamaat tawini hapo kwa kumpatia fursa ya kushiriki katika Ufunguzi huu.

Alifuatia Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nhumbili ambaye yeye alianza kwa kumshukuru Allah mtukufu kwa kupata fursa hii ya kushiriki katika ufunguzi huu ambao kwake yeye ni Historia, pia alisema kimsingi hauwezi kutembea popote Duniani ukakosa kuikuta Dini ya Kiislaam, pia akasema kuwa Mahali palipo na dini ndipo Amani inapatikana hapo, akatoa pongezi kwa Jamaat kwa kuipeleka Jamaat kijijini pale na akasema anaimani kuwa kupitia Jumuiya hii wakazi wa Nhumbili watapata mabadiliko makubwa na mazuri ya kitabia na maadili na akasema yeye yuko tayari kutoa ushirikiano wa hali na mali kwa Mwalimu wetu wa tawi hilo ili Jamii hii ipate maendeleo makubwa.

Baadae alisimama Rais wa Kanda ya Ziwa Mzee Salum Thani ambaye yeye aliwaasa wanajamaat wa hapo kwa kusema kwamba, ndugu zangu Wasukuma mmepata Msikiti, na Msikiti huu mnatakiwa muutunze na mjitahidi kufika msikitini kwa ajili ya kufanya Ibada. Akasema kwamba kumbukeni Mungu Yupo ingawa hatumwoni lakini tutambue yeye anatuona na hivyo ni wajibu wetu kumwamini inavyotakiwa, kwani tunapoviangalia vitu mbalimbali vilivyoumbwa hapa Duniani vinaelekeza kwenye Uwepo Wake, ndio maana aliwatuma Manabii ambao nao walikuja kutufahamisha uwepo wake Allah na mwishowe kabisa akaja Masih Aliyeahidiwa a.s kuja kutongoza kwenye uelekeo wa Allah.

Hivyo fahamuni kuwa nyumba (Msikiti) hii ipo hapa kwa ajili ya kumwabudu Mungu huyo. Njooni hapa Msikitini ili mumumeleze Mwenyezi Mungu matatizo yenu ili naye Awasaidieni.

Mkitaka Mafanikio ya watoto wenubasi mnatakiwa mjitahidi kuwaleta hapa Msikitiniili wapate mafunzo mazuri yatakayowasidia kupata mabadiliko na maendeleo ya kiroho na kimwili.

Baade alisimama amiri sahib kuwahutubia wanajamaat wa hapa ambapo baada ya Tashahud ,sura Fatiha na aya chache za Qur`an Tukufu , Amir Sahib aliwakaribisha wote na kuwashukuru kwa kuacha Shughuli zao na kuja pale kwa ajili ya Hafla hiyo na akasema kuwa kwa fadhila za Allah Wabashiri wetu walifika maeneo hayamiezi Kadhaa iliyopita kuja kuwapeni ujumbe wa Jamaat Ahmadiyya nanyi kwa Fadhila za Allah mkaukubali ujumbe huu wa Jamaat, hivyo ndiyo maana nimeona ni vyema kuja kuwapeni salamu na kujionea hali halisi.

Itaendelea toleo lijalo

Maana ya Kweli ya Kumshukuru Allah

Kutoka uk. 12

kujiendeleza au kuikubali kwao Ahmadiyya kulikuwa ni jambo la mpito tu na sasa wamekwama pale pale walipokuwa wamesimama zamani! Wale waliohamia katika mataifa haya yaliyoendelea wajikague pia iwapo maendeleo ya kiuchumi hayajawatenganisha mbali na imani!

Kwa fadhili za Allah, watu wengi waliohamia Denmark kutoka Kosovo na nchi zingine za Ulaya mashariki wameikubali Ahmadiyyat. Nao pia washike tahadhari kwamba hii ni baraka kubwa kutoka kwa Allah kwa wao kumkubali yule mtumishi wa kweli wa Mtume Mtukufu s.a.w.. Kwa kifupi Waahmadiyya wote, ama wawe waliozaliwa ndani ya Jumuiya au waliojiunga wenyewe baadae, wawe wale waliohamia hapa Denmark au wenye asili ya hapa, hao wote, kila mmoja, anatakiwa ajikague mwenyewe na kuona iwapo anajitahidi kutekeleza kwa matendo yake mafundisho ya kweli ya Islam, ili kutimia matakwa ya baiat aliyochukua kwa yule mtumishi wa kweli wa Mtume Mtukufu s.a.w.. Wale waliozaliwa ndani ya Ahmadiyyat, wale ambao ni Waahmadiyya wa siku nyingi, au wale walio wapya, bali Waahmadiyya wote, wanaume kwa wanawake, wanawajibika kujitathimni wenyewe iwapo wanatimiza matakwa ya Baiat au wanajitahidi kujaribu kufanya hivyo.

Je wanajitahidi kutimiza haki ya majukumu ambayo Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitarajia yatimizwe kutoka kwetu au wanajitahidi kuzifinyanga hali zao zilandane na matakwa ya Masihi Aliyeahidiwa a.s., na iwapo wanakilea kizazi chao kwa namna ambayo wanapandikiza ndani yao tabia ya kutoa kipaumbele kwa mambo ya kidini dhidi ya dunia tangu wakiwa katika umri mdogo, na iwapo matendo yetu ni kigezo kizuri kwa watoto wetu sawa na mafundisho ya Islam. Je kumuabudu kwetu Mwenyezi Mungu na kila tendo letu, linawiana na mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake s.a.w. Kila mmoja wetu anaweza kuyapata majibu ya maswali haya kwa kujichunguza na kujitafakari yeye mwenyewe. Na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametuongoza kwenye mambo haya kwa kina kikubwa kabisa.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kwamba katika zama hizi za dhoruba kali, ambapo upotofu, ujinga na kukosa mwelekeo vimezagaa kila mahala, Jumuiya yetu ni lazima ishike uchamungu. Amri za Mwenyezi Mungu hazipewi umuhimu mkubwa unaostahili na kuna kudharau kukubwa juu ya kutimiza majukumu na nasaha zinazotolewa. Watu wamezongwa na dunia kweli kweli kiasi hiki kwamba kinachoonekana kwao ni mambo ya kidunia tu! Hasara ndogo tu ya kidunia humfanya mtu aachane na imani. Hali hii inaweza kuonwa kwenye kesi mahakamani na masuala ya urithi. Mahusiano baina ya watu yamejaa uchoyo na wengi wanaonyesha udhaifu mkubwa wanapokabiliwa na matamanio yao ya kibinafsi. Hawajali kufanya kosa lolote wanapokuwa kwenye hali dhaifu, lakini hata hali yao dhaifu inapoondoka, iwapo nafasi ya kufanya kosa inajitokeza bado wanazama katika kosa hilo. Haijalishi unaangalia upande gani zama hizi, utagundua kwamba uchamungu wa kweli umetoweka na hakuna kilichobakia katika imani ya kweli. Ingawaje kwa vile Mwenyezi Mungu daima hapendi apoteze mbegu ya Uchamungu wa kweli na imani, kila anapoona shamba moja liko karibu kuangamia basi hutayarisha shamba lingine.

Kama vile Mungu mwenye Enzi Asemavyo: Hakika sisi ndio tulioteremsha mauidha haya na hakika sisi ndio tuyalindao (15:10), Quran tukufu imebakia katika usafi wake wa asili, sehemu kubwa ya Hadithi pia zimebakia kuwa sahihi kadhalika na baraka, lakini nyoyo zimepoteza imani na hakuna utekelezaji. Mwenyezi Mungu amenituma mimi ili kwamba mambo haya yahuishwe. Mwenyezi Mungu alipoona kwamba uwanja ni mweupe, kwa ghera ya Uungu wake hakuridhika na hilo la uwanja kubaki mweupe na watu kubali mbali. Hivyo sasa ili kuwasaidia wasonge mbele Mwenyezi Mungu amependa kuumba watu wapya watakaodhihirisha uhai na kwa ajili ya hilo ndio maana tunahubiri ili kwamba uchamungu uweze kufikiwa. (Paraphrased from Malfuzat, Vol. 4, pp. 395-396)

Hazrat Khalifatul Masih, akasema iwapo tutafakari yaliyotajwa juu, tutaona kwamba hayaelezi tu hali ya watu wa wakati wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. bali tunayaona hayo hayo leo hii. Ni wangapi kati yetu ambao tunashikamana na neno la Mungu kwenye maisha yetu ya kila siku, achilia mbali wengine, tujiangalie sisi ambao tunadai kumkubali Masihi Aliyeahidiwa a.s. !. Mwenyezi Mungu anasema amewaumba insi na majini ili wapate kumwabudu, je sisi tunavitoa muhanga vitu vya kidunia kwa aijili ya ibada ya Mungu au ni kinyume chake kwamba tunaitoa muhanga ibada ya Mungu kwa ajili ya vitu vya kidunia? Kuna wale ambao pia hata wanaposali Sala kwa nyakati zake hufanya hivyo haraka kana kwamba wanataka kuutua mzigo huo.

Hii ni mbali na wale ambao bado hawajamkubali Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Mwenyezi Mungu anatuagiza kuwafanyia wengine kwa wema, lakini kuna wengi kati yetu, achilia mbali kufanya wema, wao huwadhulumu wengine. Pia kuna wale ambao hawawezi kuvumilia hata hasara ndogo ya kidunia, lakini ni wavumilivu wakubwa kwenye hasara za kiroho. Pia kuna wengi miongoni mwetu ambao hawawezi kudhibiti hasira zao na wanakasirika kwa mambo madogo tu. Iwapo watu wengine watafanya haya tutasema kwamba hao ni wajinga, lakini iwapo watu miongoni mwetu wanafanya haya, hili linakuwa ni jambo la bahati mbaya kabisa. Hivyo kila mmoja wetu anaweza kujichunguza kwenye maswala haya na daima tuyaweke mbele maneno ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba Mwenyezi Mungu anapenda kuumba watu wapya watakaodhihirisha uhai. Ili kulitimiza hili ni lazima tuzingatie maneno yake.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema wakati mtu anapojitahidi kuitafuta njia ya Mwenyezi Mungu kutokana na kumhofu Mungu na kujitahidi kuomba kwa umakini katika jambo hilo, sawa na Sheria ya Mungu, kwamba Na yule anayejitahidi kwa ajili yetu, kwa yakini tunamuongoza kwenye njia zetu 29:70 Mwenyezi Mungu mwenyewe huukamata mkono wa mtu huyo ili kumuonesha njia na humpatia utulivu wa ndani wa nafsi. Lakini iwapo moyo wa mtu umejaa uovu na maombi kwake ni kitu kigumu kutamkwa na ulimi wake na anajiingiza katika kumshirikisha Mungu na vitu vingine na anajihusisha kwenye mambo ya uzushi (bidaa) katika dini, inawezekanaje maombi ya mtu huyo na kumtafuta kwake Mungu kuzae matunda!

Mtu hawi na thamani ya kupata msaada wa Mungu na kuungwa mkono na Mungu mpaka pale atakapotafuta kutoka kwa Mungu tu na akiwa na moyo safi na ikhlasi, huku akiwa amefunga milango ya njia zote na matamanio yote yasiyostahiki. Iwapo mtu atajiangusha mbele ya kizingiti cha Mwenyezi Mungu pake yake na kumuomba yeye pekee, anavutia msaada na baraka za Mungu upande wake. Mwenyezi Mungu anaziona hali za ndani za moyo wa mtu, na iwapo kutakuwa na uovu wowote au kumshirikisha Mungu na chochote, au uzushi wowote wenye madhara katika sehemu yoyote ya moyo wa mtu, maombi na ibada za mtu kama huyo anatupiwa nazo mwenyewe. Na iwapo Mungu anaona kwamba moyo wa mtu umesafika dhidi ya matamanio ya ubinafsi na uovu, humfungulia milango ya fadhili Zake na humvuta mtu huyo chini ya bawa lake na Mungu mwenyewe huchukua jukumu la kumrutubisha mtu huyo.

Mwenyezi Mungu ameianzisha Jumuiya hii au mwendeleo huu kwa mkono wake mwenyewe, na hata hivyo tunaona watu wengi wakijiunga kwa matamanio ya ovyo. Iwapo matamanio yao yanafikiwa huwa sawa kwao lakini iwapo hayafikiwi imani yao na itikadi zao huvuka mipaka. Kwa upande mwingine iwapo maisha ya masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. yatatazamwa, mtu hawezi kuona hata tukio moja la namna hiyo. Hawakuwahipo kwa namna yoyote kujiingiza kwenye mambo kama hayo. Baiat yangu ni jambo la kutubia lakini baiat ya masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. lilikuwa ni jambo la wao kujipanga kwenye mstari. Walikuwa wakifanya baiat na mara waliziacha mali zao zote, utukufu na heshima kana kwamba hawakumiliki chochote kabla ya hapo. Na hivyo walijitengenisha na matumaini na matamanio yao yote ya kidunia. Walikuwa wakiachana na mipango yao yote ya kupata utukufu, heshima na umaarufu.

Hakuna hata mmoja kati yao ambaye aliwahi hata kufikiria kwamba wanaweza kuwa watawala au washindi dhidi ya nchi zingine. Hawakuweza hata kuyafikiria mambo haya, kwa hakika walikuwa wakijiepusha na kila matamanio na walikuwa tayari kubeba kila maumivu na kila shida kwa furaha, kiasi hiki kwamba walikuwa tayari hata kuyatoa maisha yao. Kiuhalisia walijitenga na kila kitu cha kidunia. Ingawaje ni jambo tofauti jinsi Mwenyezi Mungu alivyowabariki. Aliwalipa mara elfu zaidi wale ambao walijitolea kila kitu katika njia ya Mwenyezi Mungu. (Paraphrased from Malfuzat, Vol. 5, pp. 396-398).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema wakati mtu anapoonyesha mabadiliko makubwa ya kitabia kwa jirani yake anakuwa kana kwamba anadhihirisha muujiza. Na jambo hili linabakisha athari kubwa kwa jirani yake. Kuna shutuma inayoletwa kwetu kwamba baadhi ya wanajamaat wanaonyesha kejeli na ni wenye kuchemka kwa hasira. Je si jambo la aibu kwao (kufanya hivyo) wakati wamekuja katika Jamaat hii wakidhania kwamba ni jambo jema. Mtoto mwema aliye mzuri, huling'arisha zaidi jina la mzazi wake. Mtu anayefanya baiat ni kama mtoto; na kama vile ambavyo wake wa Mtume Mtukufu s.a.w. wameitwa kuwa mama wa waaminio kana kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. ni baba wa waaminio. Baba wa kidamu hupelekea mtoto kuzaliwa duniani katika umbile la kimwili lakini baba wa kiroho humpelekea mtu kuelekea mbinguni na humuongoza mtu kwenye lengo la kweli la maisha. Je kuna yeyote kama mtoto anayependa kumtukanisha baba yake? Wajihusishe na wanawake waovu, wawe na tabia mbovu, wanywe pombe pamoja na kufanya mambo mengine ya aibu ambayo yanapelekea huzuni na hizaya kwa mzazi wake?

Mimi ninaelewa kwamba hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo? Ingawaje wakati mtoto mbaya anavyofanya hivyo, maneno maneno hayawezi kuzuiwa bali watu watanasibisha matendo mabaya ya mtoto huyu na huyu na baba huyu na huyu. Basi mtoto mbaya mwenyewe anakuwa ni sababu ya fedheha kwa baba yake. Hivyo hivyo iwapo mtu anajiunga na Jumuiya hii na kisha asijali utukufu na heshima wa Jumuiya hii na anatenda kinyume na hayo, anakuwa ni muovu mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu. Mtu kama huyo sio tu kwamba anajivutia maangamizi yake mwenyewe, lakini kwa kuonyesha mfano mbaya anawanyima wengine pia nafasi ya kuona ukweli na kuongoka. Basi tafuteni msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa nguvu yenu yote kadri muwezavyo, na jaribuni kuondoa udhaifu wenu kwa nguvu zenu na uthabiti wenu wote. Iwapo mnajisikia kushindwa, basi inueni mikono yenu kuomba kwa ukweli wa imani thabiti. Mikono inayoinuliwa kwa unyenyekevu, ukweli na imani thabiti hairudishwi mitupu. Ninasema kwa uzoefu kwamba maelfu ya maombi yangu yamekubaliwa na yanaendelea kukubaliwa.

Ni jambo la uhakika kwamba mtu ni mwenye roho chafu iwapo hana huruma kwa wanadamu. Iwapo nitaona njia ambayo ni njema, basi ni jukumu langu kuwaita watu tena na tena na kuwaeleza kuhusu hiyo na sijali kwamba watu wanaifuata au la (Paraphrased from Malfuzat, Vol. I, pp. 146-147)

Kuhusiana na ufunuo ambao Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliupokea juu ya tauni ambao unasema kwamba kila mtu atakayekuwa kwenye boma lake ataokolewa dhidi ya ugonjwa huo, isipokuwa wale wenye kiburi. Akifafanua juu ya maneno "isipokuwa wale wenye kiburi", anasema hii ni hadhari kubwa sana. Hivyo ni muhimu kukisoma kitabu cha Safina ya Nuhu mara kwa mara pamoja na kuisoma Quran tukutu na kuitekeleza. Ni nani ajuaye litakalotokea mbeleni. Mmeshasikia kila laana ambayo taifa lenu linakuombeeni. Kisha, hali yenu itakuwa ngumu na ya shida kiasi gani iwapo mahusiano yenu na Mwenyezi Mungu nayo sio safi, na iwapo hamtokuwa chini ya fadhili na baraka Zake. Ni kwa kiwango gani waandishi wa habari wanapiga kelele dhidi yetu na wanajitahidi kila wawezalo juu ya hilo. Lakini waelewe kwamba kazi ya Mwenyezi Mungu ni yenye kubarikiwa. Ingawaje ni lazima kwamba ili kupata baraka hizo tujirekebishe hali zetu kuwa bora zaidi. Hivyo jifanyieni tathmini ya imani yenu na matendo yenu. Jisafisheni dhati zetu ipasavyo ili kufikia kiwango ambacho Mwenyezi Mungu anaweza kushuka ndani ya nyoyo zenu na ili kwamba mpate msaada wake na uangalizi wake. (Paraphrased from Malfuzat, Vol. 4, pp. 69-70)

Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika kwamba unyenyekevu hufanya kazi kama mbegu ya imani. Zaidi ya hayo iwapo mtu atawacha mambo maovu basi miale laini ya imani huchomoza. Kisha wakati mtu anapojitolea mali yake kama zakat mti wa imani huchomoza matawi yake ambayo yanaiimarisha imani. Kwa kuachana na mambo ya anasa na matamanio maovu, matawi haya hupata kuimarika zaidi na zaidi na kwa mtu kuzilinda ahadi zake na amana zake mti huu wa imani unasimama juu ya kigogo chake kwa uimara zaidi. Wakati mti huu unapoanza kutoa matunda yake, hushuhudia rehema zaidi zenye nguvu kubwa ambapo bila ya rehema hizo hauwezi kutoa matunda bali hata maua. (Barahin e Ahmadiyya Part V, footnote on page 209).

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema hizi pia ni zama za mapigano ya kiroho. Vita vinaendelea dhidi ya shetani ambaye ameendelea kuishambulia ngome ya Islam kwa silaha zake zote na mbinu zake zote na anapenda kuishinda Islam. Ingawaje Mungu mwenye Enzi ameanzisha Jumuiya hii ili kumshinda shetani moja kwa moja katika vita hii ya mwisho. Wenye kubarikiwa ni wale ambao wanalifahamu hili... Karibuni zama zitafika ambapo Mungu mwenye Enzi utaufanya ukweli wa Jumuiya hii uwe wenye kung'aa kushinda jua. Hizo zitakuwa ni zama ambazo kuikubali imani hakutohesabiwa kuwa jambo la kupata zawadi za kiroho. Kwa muda huu yule ambaye ananikubali mimi analazimika kupigana na nafasi yake vita kubwa sana. Atabaini kwamba baadhi ya nyakati atalazimika kuachana na familia yake na juhudi zitafanywa ili kumzibia njia za mambo yake ya kidunia bali kidhahiri atatukanwa.

Ataendelea kulaaniwa na watu lakini Mwenyezi Mungu atamlipa malipo makubwa kwa haya yote. Lakini zile zama zingine zitakapofika na dunia kana kwamba italazimika kuielekea Jumuiya hii kama vile maporomoko ya maji yaangukavyo kutoka mlima ulioinuka juu na pale ambapo hatopatikana hata mtu mmoja wa kuipinga. Je kutakuwa na thamani gani wakati huo wa kuikubali Jamaat? Kuikubali katika nyakati hizo halitokuwa jambo la kijasiri. .. Hazrat Abu Bakr r.a. alimkubali Mtume Mtukufu s.a.w. na akafutilia mbali wazo la kuwa Chifu wa Makka lakini Mwenyezi Mungu akampa ufalme mkubwa. Hazrat Umar r.a. pia alishika unyenyekevu na akamkubali Mtume Mtukufu s.a.w. katika hali ya "litakalokuwa naliwe" na Mungu Mwenye Enzi hakumnyima chochote katika zawadi alizompangia. Iwapo mwanadamu atafanya hata juhudi ndogo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hatoondoka duniani humu bila kulipwa. Sharti ni kufanya juhudi. Hadithi inaeleza kwamba wakati mtu anapotembea kumuelekea Mwenyezi Mungu, Yeye Mwenyezi Mungu humkimbilia. Imani hasa ni kuamini kile kisichoonekana. Mtu anayeuona mwezi mwembamba siku ya kuandama huhesabiwa kuwa na jicho kali kama tai lakini yule mtu anayeshangilia kwa kuuona mwezi wakati ukiwa mpevu bila shaka mtu huyo atahesabiwa kuwa mwendawazimu.

Mwenyezi Mungu atusaidie kushikamana na amri Zake na atuwezeshe kutimiza haki za Biat. Mwenyezi Mungu atujaalie kuidhihirishia dunia njia inayoongoza kwenye ukweli kupitia matendo yetu na atujaalie sote tuonyeshe shukurani za kweli kutoka na fadhili alizotuneemesha juu yetu!

Mwisho.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Ramdh./Shawwal 1437 AH | JUNI/JULAI 2016 | Ihsan/Wafa 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na na Hadhrat Abu Huraira r.a. aliyesema ya kwamba Nabii s.a.w. alisema: Asiyeachana na kuongopa na kudanganya, Mungu hana haja ya kwamba yeye mtu huyo aache chakula chake na kunywa kwake (*Bukhari*).

Huzur aeleza Maana ya Kweli ya Kumshukuru Allah

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Katika Ijumaa hii ya tarehe 6/5/2016, Huzur Aqdas alitoa hotuba kutoka Msikiti wa Nusrat Jahan mjini Copenhagen, Denmark na alizungumzia juu ya Maana ya kweli ya kumshukuru Mwenyezi Mungu

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema kwamba ziara yake ya mwisho nchini Denmark ilikuwa miaka 11 iliyopita. Wale wote waliokuwa watoto wadogo wakati huo sasa ni vijana na wale waliokuwa vijana kwenye miaka hiyo 11 iliyopita sasa watakuwa ni wazazi wenye familia zao. Kuna baraka nyingi za wazi katika Jamaat ya Denmark. Sasa wanalo jengo la maofisi, ukumbi wa mikutano na maktaba zinazopakana na msikiti. Nyumba iliongezewa ukubwa na sasa ina makazi ya mbashiri, nyumba ya wageni na ukumbi. Hizi zote ni baraka kutoka kwa Allah. Iwapo familia za Kiahmadiyya zimestawi, kipato chao pia kimestawi, na



Nusrat Jahan Mosque Copenhagen, Denmark

Jamaat nayo imepata kustawi kwa mtazamo wa kidhahiri, jambo hili kwa hakika linatakiwa limfanye kila mmoja wetu kuwa mwenye shukurani.

Lakini ni vipi tutaweza kuidhihirisha shukurani hiyo? Sisi tuliomkubali Imam wa zama tunaamini kwamba tumemkubali yule kiongozi ambaye kumhusu huyo Mtume Mtukufu s.a.w. alisema atairejesha imani hata kama itakuwa imekwea kwenye vilimia. Hivyo nasi pia tunatakiwa tuyaelekeze mawazo yetu yaende sambamba na mawazo anayotakiwa kuwa nayo muumini wa kweli na tusitosheke tu kwa kutamka Alhamdulillah kwa mdomo. Hatuna budi tujichunguze sisi wenyewe binafsi na kuona iwapo tunayaweka maagizo ya Mwenyezi Mungu kwenye matendo yetu. Je sisi tunayapitisha maisha yetu vile ambavyo mwaminio wa kweli anatakiwa ayapitishe kama vile ilivyoelezwa na Mtume Mtukufu s.a.w., na kufafanuliwa katika zama hizi na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ?

Hazrat Khalifatul Masih alisema: Wakati wa ziara yake nchini Denmark miaka hiyo 11 iliyopita aliwakumbusha Waahmadiyya wa huko, kama vile ambavyo mara kadhaa wanajumuiya sehemu mbalimbali, na sasa kwa fadhili za Allah kupitia MTA maneno ya Huzur yanamfikia kila Ahmadiyya maadamu tu atapenda kuyasikiliza: Kwamba Mwenyezi Mungu amewawezesha wazazi wao waliotangulia kuikubali Ahmadiyya ambayo ni baraka maalum. Hivyo ni muhimu sana kwamba ili kuiendeleza baraka hii, tujitahidi kujikuza kwenye utawa na kuboresha hali zetu za kiroho. Tukishindwa kufanya hivyo tuelewe kwamba iwapo tutakwama kwenye njia yetu na kutokuheshimu maagizo ya kidini tutakiweka kizazi chetu mbali na imani na tutakinyima baraka hii maalum ambayo Mtume Mtukufu s.a.w. alitufahamisha. Iwapo kizazi chetu kijacho kitajitenga mbali na Ahmadiyya, basi nacho kitajinyima baraka za maombi yale yaliyofanywa na mababu zao walioikubali Ahmadiyya mwanzoni.

Mwenyezi Mungu kwa hakika huwalipa watu wema na kizazi chao pia hufaidika na malipo hayo, lakini Mwenyezi Mungu anasema kwamba ni lazima mtu arekebishe mwenendo wake. Mababu zetu wameondoka katika dunia hii wakiwa na matumaini kwamba familia zao zitatimiza kiapo cha ahadi ya baiat. Wanajumuiya wote wa Denmark wanatakiwa wajikague iwapo wanatimiza matakwa ya kiapo cha hadi ya Baiat kwa roho yake ya kweli. Inahitajika kwa kila mmoja wao kujikagua iwapo anatimiza ahadi za baiat kwa ukweli halisi au kwa sababu ya fungamano za kifamilia na kijamii tu. Wakati huo huo wale ambao wameikubalia Ahmadiyya wao wenyewe nao pia wanatakiwa wajichunguze ili kuona kwamba baada ya kujiunga wamejiendeleza katika kukuza imani yao au wanajaribu

Endelea uk. 11

Ziara ya Amir sahib pamoja na ufunguzi wa Misikiti minne mkoani Shinyanga

Na Mwandishi wetu
Shinyanga

Baada ya kumalizika kwa Mkutano wa Mwaka wa Kanda, Tar 23/05/2016 siku ya Jumatatu Amir Sahib akiambatana na viongozi mbali mbali wa Jamaat alianza Ziara ya Siku tano katika Mkoa wa Shinyanga ambapo pamoja na kukutana na Wanajamaat katika Matawi yao na kuzungumza nao na kujionea hali halisi ya wanajamaat na Jamaat kwa ujumla, alipata pia fursa ya kufungua misikiti minne na kuweka jiwe la Msingi la Ujenzi wa Msikiti katika Jamaat mpya ya Kasomela Wilaya ya Ushetu Mkoani Shinyanga.

ZIARA NA UFUNGUZI WA MSIKITI WA JAMAAT TAWI LA BUCHAMA.

Siku ya jumatatu tar 23/05/2016, Msafara wa Amir Sahib pamwe na wajumbe wake ulifika kijijini Buchama saa sita na nusu mchana ambapo alipokelewa na wanajamaat wa Buchama wakiongozwa na Mwl wa matawi ya Nhumbili na Buchama.

Baada ya mapokezi na



Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akizindua moja ya misikiti iliyojengwa hivi karibuni mkoani Shinyanga

salaam ilifuatia Sherehe fupi iliyoandaliwa na Wanajamaat wa Buchama kwa Mtiririko ufuatao;

Ilianza usomaji wa Quran Tukufu iliyosomwa na Mwl Shiraaz ud din Hamza na baadae ilifuatiwa na risala ya Wanajamaat wa tawi hilo ambapo katika Risala yao pamoja na Kumkaribisha Amir sahib walimueleza Amir sahib haya yafuatayo,

Walisema kuwa wao walijiunga na Jamaat tangu mwaka 2014 mwezi December ila hawakupata malezi kutokana na uhaba wa waalimu,

Pia walitoa shukurani kwa kujengewa msikiti lakini walieleza kuwa wakati wa ujenzi wa msikiti walijitolea kusaidia mafundi na pia kuwaletea maji mafundi. Pia walijitolea kuchimba msingi wa ujenzi wa msikiti huo.

Walimuomba Amir sahib awapatie mwalimu wa kudumu katika tawi hilo ili wapate malezi kwa ukaribu zaidi.

Baade alikaribishwa Mwenyekiti wa Kitongoji ambaye yeye alitoa salaam na kuishukuru Jamaat kwa kuwajengea msikiti wakazi wa Buchama.

Baadae Afisa Afya wa Kijiji nae alipewa nafasi na baada ya kutoa Salaam na Shukurani kwa ujio wa Amir sahib, aliwahimiza wakazi wa kijiji hicho kuzingatia kanuni za usafi wa Mazingira pamoja na kuutunza Msikiti huo. Pia alisistiza umuhimu wa kumcha Mungu ili wawe waumini wema.

Baadae alipewa nafasi Kamanda wa Sungusungu ambapo yeye alisimama na kutoa Salaam pamoja na Pongezi kwa Amir sahib kwa kuwatembelea wakazi wa Kijiji hicho.

Ilifuatia khutba iliyotolewa na Mwl Ame sahib ambapo baada ya salaam na Tashahud na Kumhimidia Allah, alitambua uwepo wa viongozi wa

Endelea uk. 10